SportPesa
TZS. 559,183,880
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mwalimu** wa madrasa mbaroni kwa tuhuma kudhalilisha watoto

UKURASA 17


Harakati za 50/50 wanawake sasa kuzifikisha mitandaoni
Makamu wa Pili wa Rais SMZ anapobua wajibu wa wanaCCM uchaguzi 2025
siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Watuhumiwa uhalifu wa binadamu wanaotamba na nishani za Nobel
Mwanaharakati: Rahisi kwa mama kushika uongozi juu, kuliko chini

UKURASA 11



# Nipashe

Jumatano Oktoba 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580725

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/thegua



# Nafuu bei ya petroli, dizeli

**Rais** Samia aagiza tozo zishushwe kwa manufaa ya umma... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

## MAWAZIRI WAANZA KAZI UTATUZI MIGOGORO ARDHI

KAMATI ya mawaziri wanane iliyopewa maagizo maalum na Rais Samia Suluhu Hassan ya kushughulikia migogoro kati ya wananchi na hifadhi...

UKURASA WA 4

## SERIKALI KUJENGA MTANDAO RADA 7

SERIKALI imeingia mkataba kwa ajili ya ujenzi wa rada mbili za mwisho za hali ya hewa ili kufikisha mtandao wa rada saba zinazofungwa katika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro...

UKURASA WA 4

## HUKUMU YA AVEVA, KABURU KISUTU LEO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu leo inatarajia kutoa hukumu dhidi ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na...



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na baadhi ya mawaziri akiwamo wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, Nishati, Januari Makamba pamoja na baadhi ya watendaji wa taasisi mbalimbali za serikali, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Marekani yatoa fursa visa uhamiaji kwa Watanzania

UKURASA 2

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimsikiliza Waziri mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Benard Membe, wakati akitoa salamu, katika viwanja vya Shule ya Sekondari Mnara, Londo, Jimbo la Mtama, mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**



# Sweden yamwaga bil. 195/- elimu

UKURASA 3

**MICHEZO** TAMBWE ATAMBA KUWASHA MOTO AKIANZA NA MABAO 4 UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Nafuu bei ya petroli, dizeli

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameelekeza kupunguzwa kwa tozo zinazotozwa na taasisi mbalimbali katika bidhaa za mafuta nchini zenye thamani ya Sh. bilioni 102 kwa mwaka, kwa lengo la kupunguza bei za mafuta ili kuwapa unafuu wananchi.

Alitoa maagizo hayo jana akipokea taarifa kutoka kwa Waziri wa Nishati, January Makamba, kuhusu utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa kwa wizara hiyo kupitia mwenendo wa biashara ya mafuta na bei zake nchini.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu jana kwa vyombo vya habari ilibainisha kuwa utekelezaji wa maagizo hayo umeenda sambamba na marekebisho ya kanuni mbalimbali zinazohusiana na tozo na taarifa zilirajiwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali jana.

Ilibainishwa katika taarifa hiyo ya Ikulu kuwa Rais Samia amechukua hatua hiyo ili kukabiliana na upandaji wa bei za mafuta katika soko la dunia ambapo kwa muda mrefu imekuwa ikipanda kwa kiwango kikubwa na kuathiri watumiaji wa bidhaa hiyo nchini.

Taasisi zinazoguswa na maelekezo ya kupunguzwa kwa tozo hizo ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (tozo ya udhibiti), Mamlaka ya Bandari (tozo ya miundombinu), Mamlaka ya Mapato Tanzania (tozo ya kuchakata taarifa) na Shirika la Viwango Tanzania (tozo ya kupima ubora wa mafuta kwenye meli na gharama ya uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta).

Zingine ni Wakala wa Vipimo Tanzania (tozo ya uhakiki wa ujazo wa mafuta melini), Wakala wa Usimamizi wa Meli (tozo ya forodha) na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (ushuru wa huduma kwenye halmashauri nne zenye maghala ya kupokea mafuta kwa jumla). Halmashauri hizo ni Kigamboni na Temeke za mkoani Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Rais Samia pia ameagiza ufanyike mchakato wa haraka wa kupeleka marekebisho ya sheria bungeni endapo zipo sheria zingine zinazohitaji marekebisho ya haraka katika kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta nchini, ili kumlinda Mtanzania dhidi ya gharama za maisha zinazotokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

**UFAFANUZI EWURA**

Jana jioni, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, akitangaza bei mpya za mafuta kwa mwezi Oktoba ambazo zinaanza leo, alisema mjini Dodoma kuwa kupunguzwa na kufutwa kwa baadhi ya tozo kutasaidia kutokuwa na ongezeko kubwa la bei za mafuta.

Alisema bei mpya ya petroli kwa Dar es Salaam imeongezeka kwa Sh. 12 badala ya Sh. 145 kwa lita iliyotakiwa kuongezeka kuanzia leo.

"Dar es Salaam lita ya mafuta ya petroli ni Sh. 2,439, dizeli Sh. 2,261, mafuta ya taa Sh. 2,188. Kwa Arusha lita ya petroli ni Sh. 2535, dizeli Sh. 2,301 na mafuta ya taa ni Sh. 2272. Pwani lita ya petroli ni Sh. 2,443, dizeli Sh. 2,226, mafuta ya taa Sh.2,192 huku Dodoma itakuwa petroli lita moja ni Sh. 2,497, dizeli Sh. 2,320 na mafuta ya taa Sh. 2,246," alibainisha.

**MTAZAMO WA WACHUMI**

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kutangazwa kwa uamuzi huo wa serikali, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi, alisema ni wazi kuwa uamuzi huo umechukuliwa kutokana na kubainika kuwa bei ya mafuta ipo juu, hivyo inamuumiza mtumiaji wa mwisho.

"Ni hatua nzuri maana kushuka kwa bei ya mafuta kunasababisha hata gharama za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ambazo mashine zinatumia mafuta hayo kuendelea kuuzwa kwa bei ambayo wengi wanamudu," alisema.

Hata hivyo, Prof. Ngowi alisema kwa upande mwingine hatua iliyochukuliwa na serikali inakwenda kuziathiri baadhi ya taasisi zinazotegemea tozo hizo katika mapato yake, hivyo serikali italazimika kuzisaidia kifedha.

***Imeandikwa na Augusta Njoji (DODOMA) na Beatrice Moses (DAR)**




Mkurugenzi wa IPP, Abdiel Mengi akipata chanjo ya Uviko-19, wakati wa zoezi lililoendeshwa na wataalamu wa afya kwa wafanyakazi wa IPP Media, kwenye viwanja vya EATV, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Zoezi hilo, liliienda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu ugonjwa huo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafanyakazi IPP wachanja corona

**Na Romana Mallya**

WAFANYAKAZI wa vyombo vya habari vya IPP, wamejitokeza kuchanja chanjo ya corona, huduma hiyo ilipotolewa ofisini kwao Mikocheni, Dar es Salaam.

Chanjo hiyo iliendeshwa jana na wahudumu wa afya kutoka Kituo cha Afya Magomeni kwa niaba ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Baadhi ya wafanyakazi waliopata chanjo hiyo, walielezea kufurahishwa na huduma iliyotolewa huku wakishauri watu wajitokeze kuchanjwa ili kuepuka na maradhi ya corona ambayo yamekuwa yakigharimu mamia ya Watanzania

Mhariri wa Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago, aliwataka wananchi kujitokeza kupata chanjo na kueleza kuwa haina madhara huku akielezea kufurahishwa na huduma iliyotolewa na watumishi hao wa afya.

"Wanaobisha au kupinga chanjo hawajaona madhara ya corona au hawajafiwa au kuuguza. Chanjo haina madhara inakuchukua muda mfupi mwili wako unarudi katika hali ya kawaida," alisema.

Meneja wa Matangazo wa Kampuni ya The Guardian Limited, Angel Navuri, aliwahamasisha vijana wawe mstari wa mbele kuchanja kwa sababu wao ndio nguvu kazi ya taifa.

"Hutaki kuchanja lakini tukumbuke dunia inakokwenda utachanja tu kwa sababu zipo fursa mbalimbali duniani ambazo kama kijana lazima uzitafute. Kuchanja ni kujikinga na ukijikinga wewe utaikinga familia yako," alisema.

Mwandishi wa habari, Faustine Feliciane, alisema amechanja na hajapata madhara yoyote ambayo alikuwa anayasoma kwenye mitandao ya kijamii.

"Chanjo ni salama haina madhara yoyote. Tukachanje, ninawahamasisha vijana wenzangu wenye umri wa kuchukua chanjo wafanye hivyo, wasiogope. Tukichanja wengi tutaliepusha taifa na maambukizi zaidi," alisema.

# Marekani yatoa fursa visa uhamiaji kwa Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani jijini Dar es Salaam unatarajia kuanza programu ya kupokea maombi ya visa mbalimbali (Diversity Visa) kwa mwaka 2023 kuanzia kesho.

Taarifa iliyotolewa na ubalozi huo jana, ilisema

kila mwaka, kupitia programu hiyo, Marekani hutoa visa za ukaazi wa kudumu (immigrant visas) zipatazo 55,000 kwa raia wa nchi ambazo kihistoria zina idadi ndogo ya watu wanaohamia Marekani.

Taarifa hiyo iliwataka Watanzania wenye sifa kutuma maombi yao katika programu hiyo ya uhamiaji kabla ya Novemba 9, 2021.

Ubalozi huo umeweka tovuti maalumu; https://travel.state.gov/content/travel/en/us-visas/immigrate/diversity-visa-program-entry/diversity-visa-instructions.html ya maombi ya kupata viza hiyo katika kipindi cha mwaka 2023 (DV-2023) ambayo yatapokelewa kuanzia Oktoba 6, saa 6 mchana kwa saa za Marekani Mashariki (EST) hadi Novemba 9, 2021 saa 6 mchana kwa saa za Marekani Mashariki (EDT).

Pia waombaji wametakiwa kujaza fomu maalumu ya kielektroniki ya kuomba kushiriki katika programu ya Diversity Visa (E-DV Entry Form au DS-5501) inayopatikana kupitia dvprogram.state.gov.

"Unaweza kutuma ombi lako mara moja tu, katika kipindi kilichotajwa na kwa njia ya mtandao pekee. Maombi yaliyochelewa au yatakayoletwa kwa njia ya barua/karatasi hayatapokelewa." Ilisema taarifa hiyo.

Kadhalika waombaji wametakiwa kuzingatia kuwa hakuna ada yoyote inayotozwa kwa kutuma maombi kupitia mtandao.

Mwombaji asitume, asilipe wala kuhamishia fedha kwa taasisi au mtu yeyote anayedai anaweza kumsaidia kupata viza hiyo.

Vilevile, mwombaji atalazimika kuingia katika mtandao wa internet ili aweze kujua kama atakuwa amechaguliwa kuendelea na mchakato wa visa hiyo. Mfumo wa kueleza matokeo ya Diversity Visa utapatikana katika tovuti ya dvprogram.state.gov kuanzia Mei 8, 2022, hadi Septemba 30, 2023.

Taarifa hiyo ilisema iwapo mtu atakuwa amepata Diversity Visa, atatakiwa kulipia ada ya maombi ya viza katika Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam wakati atakapoitwa kwa ajili ya usaili wa viza.


Kama kuna mtu yeyote atadai fedha kwa ajili ya kusaidia kuingia katika programu hiyo, mwombaji awasiliane na Ubalozi wa Marekani.

Hata hivyo, taarifa hiyo imefafanua kuwa mtu kuchaguliwa kwa maombi ya Diversity Visa, haimhakikishii moja kwa moja kupata viza. Bado atahitajika kusailiwa ili kuona kama anakidhi vigezo vya sheria ya Uhamiaji wa Marekani.

Kadhalika, mwombaji anaweza kuwajumuisha watu wa familia yake (mke/mume na watoto wako wa kuwazaa ambao bado hawajaoa au kuolewa walio chini ya miaka 21) katika maombi ya viza hiyo.

Mwombaji atatakiwa kuorodhesha watu wote wa familia yake (immediate family) katika maombi hata kama wasingependa kuhamia Marekani pamoja naye. Kushindwa kufanya hivyo kutasababisha kukosa sifa na maombi kukataliwa wakati wa usahili wa viza.

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba na Balozi wa Sweden hapa nchini, Anders Sjoberg, wakibadilishana nyaraka baada ya kutiliana saini mkataba wa msaada wa Sh. bilioni 195.9 kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Elimu kwa Matokeo (EPforR II), jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mwanasheria wa wizara hiyo, Nyanzala Nkinga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sweden yaipa Tanzania bil. 195/- sekta ya elimu

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA imepokea msaada wa Krona milioni 750 (Sh. bilioni 195.9) kutoka serikali ya Sweden, kusaidia sekta ya elimu.

Msaada huo ni awamu ya pili ya Mpango wa Elimu kwa Matokeo (EPforRII).

Mkataba huo ulisainiwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba na Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjöberg.

Tutuba alisema mpango wa EPforRII utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia Julai mwaka huu hadi Juni mwaka 2026, kwa lengo la kuongeza ubora katika elimu ya msingi.

Aliongeza kuwa katika awamu ya kwanza ya EPforRI, Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Kimataifa la Maendeleo (SIDA), ilichangia Sh. bilioni 207.7.

Tutuba alisema Agosti 26, mwaka huu Tanzania na Sweden zilitia saini mkataba wa msaada wa SEK milioni 450 (Sh. bilioni 117.6) kwa ajili ya Mpango wa Pili wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN II).

Kwa mujibu wa Tutuba, EPforR unachangiwa na wafadhili mbalimbali wakiwamo FCDO, Benki ya Dunia (WB), SIDA, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA) na Shirika la Elimu Duniani (GPE) kwa kutumia mfumo wa mpango kwa matokeo kuleta mabadiliko yenye tija katika sekta ya elimu msingi Tanzania.

Aidha, aliyataja baadhi ya mafanikio ya EPforRI kutoka mwaka 2014/2015 hadi 2020/2021 ni ujenzi wa madarasa 10,409, vyoo 20,507, mabweni 646, nyumba za walimu 91, majengo ya utawala 37, maktaba 49, maabara 29, uzio katika shule tatu na uchimbaji wa visima vya maji katika shule 16.

Mengine ni ujenzi wa ofisi 155 za udhibiti wa ubora wa shule na kuweka vifaa na kuboresha mazingira ya kazi na kusogeza karibu huduma kwa wateja wa shule za msingi na sekondari.

Pia ujenzi wa shule mpya 44, ukarabati wa shule kongwe za serikali 86 na ukarabati wa ofisi 31 za udhibiti wa ubora wa shule.

Balozi Sjöberg, alisema lengo kuu la SIDA ni kutengeneza fursa kwa watu wanaoishi kwenye umaskini na ukandamizaji ili kuboresha maisha yao, hivyo kwa Tanzania elimu ni moja ya malengo muhimu katika mkakati wa Sweden.

Alisema Tanzania na Sweden zimekuwa zikishirikiana katika sekta ya elimu tangu mwaka 1960, kwamba mchango wao kwenye sekta hiyo umekuwa wa uwekezaji mkubwa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema msaada huo utasaidia upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wa Tanzania.

# Mawaziri waanza kazi utatuzi vijiji vyenye migogoro ya ardhi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya mawaziri wanane iliyopewa maagizo maalum na Rais Samia Suluhu Hassan ya kushughulikia migogoro kati ya wananchi na hifadhi kwenye vijiji 920 nchini, imeanza kazi kwa kupitia vijiji 42 huku viwili vikiondolewa wilayani Chemba ili kupisha mradi wa Bwawa la Maji la Farkwa

Pia vijiji 20 kati ya hivyo vitapimwa na kufanyiwa tathmini upya ili kuangalia kama kuna vikwazo kwa kuwa ni mali ya wananchi. Vijiji hivyo viko katika wilaya za Chemba, Bahi na Kondoa.

Akizungumza jana jijini hapa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema vijiji 40 vilivyosajiliwa vitabaki lakini viwili vitaondolewa ili kupisha ujenzi wa bwawa hilo.

Alisema baadhi ya vitongoji vyenye vikwazo kwenye vijiji hivyo vya mradi lazima wananchi wapishe ili mradi uanze kwa kuwa fedha ziko tayari.

"Kati ya vijiji hivyo 40, 20 havina shaka lakini 20 vilivyosalia kutokana na maelekezo ya Rais vifanyiwe tathimini, tumeunda timu itakayohusisha watendaji wa hapa kwa kushirikisha wananchi wapitie na kushauri nini kufanyike na baadaye tutatoa maelekezo," alisema.

"Tunaomba mkishafanya tuambieni hapo kweli kuna mazalia ya wanayama au kuna kitu gani cha kuhatarisha maisha ya wananchi wa eneo hilo na kama tunatakiwa kuwaondoa wananchi kwa sababu gani," aliongeza.

Lukuvi alisema kwenye eneo la pori la Mkungunero kuna mgogoro wa muda mrefu hali iliyowalazimu kuunda timu maalumu kuchunguza na tayari imewasilisha majibu, hivyo kwa sasa kinachofanyika ni kutafakari upya ili kuondoa kasoro zilizopo ikiwamo uundwaji wake.

Alifafanua kuwa kuna baadhi ya vijiji vimesajiliwa Mkoa wa Manyara lakini vimevuka mpaka hadi Dodoma wakati ilitakiwa viwe Wilaya ya Kondoa tu.

"Kuna vijiji vinapata hadi Sh. bilioni moja kutokana na uwindaji hali inayosababisha eneo husika kukosa fedha. Lazima tuendelee kuyalinda na kuyapima maeneo upya ili kuona namna ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza," alisema.

Pia alisema tayari serikali imeshafuta mapori tengefu 12 yenye hekari 700,007 na misitu ya hifadhi saba kutokana na kupoteza sifa kutokana na kuvamiwa na wananchi na baadhi yapo Mkoa wa Dodoma.

Ofisa Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Herman Kiryario, alisema maeneo yaliyotembelewa Mkoa wa Dodoma kwa jana ni vitongoji vya Ilala A, Ilala B na Mnang'ana vilivyoko kijiji cha Handa.

Alisema mawaziri hao wa kisekta walitembelea kitongoji cha Mbugani kijiji cha Handa katika Hifadhi Pori la Swagaswaga, Bubutole na Mombose ambapo ulitumika usafiri wa helikopta.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi(CCM) Mkoa wa Dodoma, Pili Mbanga, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi wa kuhakikisha migogoro hiyo inafanyiwa tathimini kwa wakati.

Alisema mwaka 2024 kwenye uchaguzi wa serikali za vijiji na mitaa hivyo wataenda kifua mbele na kushinda kwa kishindo.

"Kero zote za migogoro zitakuwa zimeisha, na sisi kama chama tunafarijika na tutashiriki ili tukiulizwa kuhusu masuala haya na wananchi tuwe na majibu," alisema.


GSP AUCTION MART
P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. AFCL/2021/DM/028**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L. P 40780 Dar es salaam,** tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa ya tarehe 15/10/2021 na **tarehe 29/10/2021**. Mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| MICHAEL WILLIAM KILIWA | LPT 1116 | T533 DSP | DAR ES SALAAM |
| GEORGE JACKSON BALAZI | LX PRIMA | T701 DPW | DAR ES SALAAM |
| SALIM GROUP LIMITED | LP 909 BUS | T785 DPH | DAR ES SALAAM |
| JOSHUA GODWIN MSESA | LP 909 BUS | T326 DSN | DAR ES SALAAM |
| CCS POWER SOLUTION(T) LIMITED | LP 909 BUS | T749 DPB | DAR ES SALAAM |
| TAI DIVE LIMITED | LPK 2518 TIPPER | T590 DSM | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

216491201



bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **BEATUS ASSEY** | **ALBINA TESHA** | Nyumba ya makazi yenye Hati ya usajili na.86073 Kiwanja na.5 kitalu"S" iliyopo Goba Tegeta | 30/10/2021 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: AU**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

116493802

# Hukumu ya Aveva, Kaburu leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu leo inatarajia kutoa hukumu dhidi ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na Makamu wake, Godfrey Nyange maarufu Kaburu.

Uamuzi huo ulifikiwa Septemba 30, mwaka huu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba baada ya washtakiwa kufunga ushahidi wao wa utetezi.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo ulikuwa na mashahidi 10 na wa utetezi mashahidi wawili ambao ni washtakiwa.

Katika kesi hiyo washtakiwa walikuwa watatu, Aveva, Kaburu na Zackaria Hanspope ambaye alifariki Septemba 10, mwaka huu.

Washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka saba likiwamo shtaka la matumizi mabaya ya madaraka.

Katika shtaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Mshtakiwa Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko Benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko Benki ya Barclays.

Pia Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja walighushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva kitu ambacho sio kweli.

Aveva anadaiwa katika Benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000.

Aveva anadaiwa kuwa katika Benki ya Barclays Mikocheni alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na marehemu Hans Poppe walikuwa wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba sio kweli

Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.

Pia Aveva, Kaburu na Hanspope wanadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kuonyesha kuwa Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa (wa pili kulia), wakati wa kongamano la tano la uwezeshaji lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), jijini Dodoma jana. Kutoka (wa pili kushoto) ni Meneja wa Tawi la DCB Dodoma, Daniel Buzuka, Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Steven Ndaki na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Generali Wilbert Ibuge. DCB ilikuwa moja ya wadhamini wa kongamano hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafurahia kusogezewa chanjo ya Uviko-19

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

WANANCHI wa vijiji vya Ngalawale na Kilimahewa wilayani Ludewa mkoani Njombe wamefurahia kusogezewa huduma ya chanjo ya Uviko-19 kupitia mikusanyiko na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu.

Alisema awali umbali ndiyo ulikuwa sababu ya wao kutochanjwa pamoja na ukosefu wa elimu ya chanjo.

"Tumefurahia kusogezewa huduma hii ya chanjo kwa kuona gari la watu wa afya likifika hadi kwenye kijiji chetu, hii imetupunguzia kutembea umbali mrefu kufuata chanjo hii katika vituo vilivyopangwa kwa ajili ya kupata huduma hii, hapa Ludewa ipo kwenye hospitali ya wilaya ambako ni mbali," alisema Martha Haule.

Garusi Mwinuka, mkazi wa kijiji cha Kilimahewa, alisema alikuwa akisubiri kwa hamu kupata chanjo hiyo pamoja na kupewa cheti kwa madai yeye ni mfanyabiashara anayesafiri mara kwa mara na kupata cheti cha chanjo kutamuondolea usumbufu wakati wa kusafiri.

"Nawashauri ambao hawajapata chanjo hii wasisite, mimi sijaona kama kuna shida yoyote iliyojitokeza kwangu, hakuna kabisa maudhi ambayo pengine nilifikiria yangenikuta," alisema Mwinuka.

Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Wilaya ya Ludewa, Dk. Leisleyi Mhagama, alisema uamuzi wa kutoa elimu ya chanjo ya Uviko-19 wanaufanya kwa lengo la kuihamasisha jamii kuondokana na dhana potofu kuwa chanjo hiyo si salama.

"Chanjo sio lazima lakini tunawatoa shaka wananchi waendelee kupata chanjo ya Uviko-19 kwa kuwa haina tatizo lolote na inasaidia kutopata maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa kiwango kikubwa tofauti na mtu akiwa ameambukizwa ugonjwa huo," alisema Mhagama.

Kwa upande wake, James Kadege, mratibu wa chanjo Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, alisema licha ya kutoa huduma hiyo katika vituo vyote vya afya, umbali uliopo katika maeneo ya kutolea huduma ya chanjo kwa wananchi umesababisha wilaya kutoa huduma hiyo kwa njia ya mkoba kwa kutembea kaya kwa kaya ili kuwafikia wananchi wanaotaka kupata chanjo.

## Watano wauawa wakijaribu kuteka gari la polisi

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

WATU watano wanaodaiwa kuwa majambazi waliokuwa na mabomu ya kutupa kwa mkono na mapanga wameuawa na Jeshi la Polisi mkoani Kigoma wakati wakijaribu kufanya tukio la kuliteka gari la polisi.

Akithibitisha tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema juzi majira ya saa tano usiku polisi wakiwa kwenye doria barabara ya Kasulu- Kibondo, jirani na kambi ya wakimbizi ya Nduta walisimamishwa na majambazi hao waliokuwa wamepanga mawe na magogo barabarani. Alisema watu hao awali hawakulitambua gari hilo kuwa ni la polisi kutokana na kuwa na namba za kawaida na kuamrisha askari hao kushuka chini na walipobaini kuwa ni askari ikawabidi warushe bomu la kutupa kwa mkono ambalo hata hivyo halikulipuka.

Alisema askari walijibu mapigo kwa kuwafyatulia risasi na watu wawili kuuawa papo hapo huku wengine watatu wakijeruhiwa na kupoteza maisha wakiwa njiani kuelekea hospitali.

Kamanda Manyama alisema upekuzi eneo la tukio hilo ulibaini uwapo wa mabegi mawili yenye mabomu mengine mawili ya kutupa kwa mkono na mapanga matatu pamoja na dagaa.

"Bado tunafanya uchunguzi kubaini kama vijana hawa wametoka kambi za wakimbizi au la, jeshi la polisi hatuta rudi nyuma hakika tutawamaliza," alisema Kamanda Manyama.

## Serikali kujenga mtandao rada 7

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeingia mkataba kwa ajili ya ujenzi wa rada mbili za mwisho za hali ya hewa ili kufikisha mtandao wa rada saba zinazofungwa katika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha ukusanyaji na utoaji wa taarifa za hali ya hewa nchini.

Tayari serikali imeshafunga rada tano za hali ya hewa, tatu zikifungwa katika mikoa ya Dar es Salaam (Bangulo), Mwanza (Kiseke) na Mtwara (Mikindani).

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana Dar es Salaam alipotembelea Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ambapo pamoja na mambo mengine, alipongeza mamlaka hiyo kwa ufanisi na utendaji kazi mzuri ndani na nje ya nchi.

Waitara alisema rada hizo tayari zimeshaanza kufanya kazi na rada mbili zinazofungwa katika mikoa ya Mbeya (Kawetire) na Kigoma (Nyamoli) ziko katika hatua za mwisho za utekelezaji.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TAARIFA KWA UMMA

## UNUNUZI, UUZAJI NA USAJILI WA MAGARI BILA KUFUATA TARATIBU NA UHAKIKI KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO

Kwa kuzingatia Kifungu Na. 117, 119 na 200 vya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004, **ikisomwa kwa pamoja na Kifungu Na. 11 cha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973,** Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuufahamisha na kuukumbusha umma kufuata taratibu zilizoanishwa kwa mujibu wa sheria wakati wa ununuzi, uuzaji na uhamishaji umiliki wa magari kabla ya kupata usajili wa magari hayo. Hapa siku za karibuni tumebaini ukiukwaji wa sheria katika maeneo yafuatayo:-

1. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Msamaha wa Kodi**
   Mtu yeyote anayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa gari ambalo lina msamaha wa kodi, anapaswa kufika ofisi ya karibu ya Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kujua kiasi cha kodi anachopaswa kulipa kabla ya kununua na kubadili umiliki. Kutumia gari hilo bila kufuata utaratibu huu ni kosa kisheria.

2. **Magari Yaliyoingizwa Nchini kwa Hati ya Muda Mfupi (Temporary Import)**
   Magari yote yalioyoingizwa nchini kwa hati ya muda mfupi kwa lengo la utekelezaji wa shughuli maalum iliyoidhinishwa kwa mujibu wa sharia kama iliyotajwa katika Kifungu Na. 136 cha sheria iliyotajwa hapo juu, yakiwemo magari binafsi, yamepewa muda maalum wa ukamilishaji wa shughuli hiyo ya kuwepo kwao hapa nchini. Wananchi wote pamoja na waigizaji wa magari hayo, wanatahadharishwa kuwa muda huo ukiisha yanapaswa kurudishwa nchi yalikotoka. Kuendelea kutumia magari hayo nje ya muda ulioanishwa ni kosa kisheria.

   Aidha, yeyote atakayehitaji kuuza, kununua au kubadili umiliki wa magari hayo ni lazima afike ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya uhakiki na kupewa taratibu za kufuata,

3. **Magari Yaliyoingizwa Nchini Kinyume na Sheria**
   Haya ni magari yaliyoingia nchini bila ya kufuata taratibu, ama kwa njia ya magendo ama Transit. Tunawakumbusha wote wanaoingiza magari nchini kufuata taratibu zilizowekwa ikiwemo kupita katika njia zilizoainishwa.

**Kwa mantiki hiyo:** Wananchi wote wanashauriwa kuwa wanapotaka kununua gari yoyote, kudai nyaraka zilizotumika kuingiza gari hiyo nchini. Aidha wanunuzi hao wanatakiwa kuhakiki nyaraka hizo katika ofisi za TRA zilizo karibu.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi**
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Walipakodi**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216489002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uporaji mali ajalini ni uhalifu, udhibitiwe

**KUNA** matukio ambayo yanaendelea kwa kasi katika maeneo yote ya Tanzania, ambayo wananchi wanapora mali za abiria zinapotokea ajali barabarani.

Kadhalika, wananchi hao wanavamia magari ya mizigo na kupora mali baada ya kutokea ajali. Tumekuwa tukishuhudia uporaji huo malori yanapoanguka na kodondosha bia, soda, saruji na wakati mwingine kuchota mafuta kwa kutumia madumu, ndoo na vifaa vingine.

Kibaya zaidi ni kwamba wananchi hao wanawapekua majeruhi na hata maiti kwenye mifuko na kuwanyang'anya fedha badala ya kuwapa msaada ikiwamo kuwapeleka hospitali au kuwahifadhia mali zao,

Vitendo hivyo hivi sasa vinaonekana kama vya kawaida, lakini ukweli ni kwamba ni uhalifu kama mwingine, ambao vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinapaswa kuuchukuliwa hatua.

Yametokea matukio mengi ya aina hi na la karibuni ni la juzi Mbagala Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo wananchi walivamia lori la saruji na kuanza kuiba saruji baada ya kupata ajali katika eneo la Misheni, Mtaa wa Kizinga.

Kwa mujibu wa mashuhuda waliokuwa eneo hilo, baada ya lori hilo kufika eneo la Misheni lilifeli breki na kuanza kuteremka chini kwenye makazi ya watu na kugusa daladala mbili kwa upande wa nyuma pamoja na nyumba.

Kwamba ndipo wananchi hao walivamia na kuanza kuchukua mali za watu waliokuwamo katika lori hilo pamoja na kuanza kuiba saruji.

Kutokana na jinsi ambavyo wananchi walikuwa wakitumia nguvu nyingi kupora saruji na mali nyingine, waliokuwamo kwenye lori iliwabidi wakimbie kwa ajili ya kuokoa maisha yao.

Miaka iliyopita yalitokea matukio mengi ya aina hiyo, ambayo yalisababisha vifo vya baadhi ya wananchi waliokuwa wakijaribu kupora mali baada ya ajali. Kwa mfano, mkoani Mbeya watu kadhaa walikufa walipokuwa wakichota mafuta baada ya lori kuanguka.

Mwaka juzi takribani 100 walikufa katika Manispaa ya Morogoro kwa kuungua walipokuwa wanachota mafuta, huku baadhi wakiwa ni wapiti njia baada ya lori la mafuta kuanguka.

Mwendelezo wa vitendo hivi vya kikatili sio tu kwamba vinasababishwa na umaskini miongoni mwa Watanzania, bali ni tamaa ya kutaka mali bila kufanyakazi pamoja na kutokuwa na hofu kwa Mungu.


Kutokana na hali hiyo, tunashauri kwamba sasa ni wakati mwafaka kwa jamii kuvichukia vitendo hivyo, ambavyo kama havitadhibitiwa, upo uwezekano wa kushuhudia majeruhi na abiria wengine wakidhuriwa na watu hao ambao hawathamini uhai wa binadamu.

Inawezekana wananchi wengine wanajiingiza kwenye uporaji huo kwa mkumbo bila kujua kuwa huo ni uhalifu, hivyo tunashauri kwamba zichukuliwe hatua, na kwa kuanzia utoaji wa elimu kwa umma hususan kwa wakazi wanaoishi katika maeneo ya barabara.

Nyingine ni kwa mamlaka zinazohusika na utekelezaji wa sheria hususan vyombo vya dola kuzitumia sheria zilizoko kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wote watakaobainika wakipora mali kwenye ajali.

Tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo, ukubwa wa tatizo hili utapungua, hivyo abiria na bidhaa zinazosafirishwa kufika salama. Udhibiti huo pia utawaepusha wananchi kuepukana na majanga ambayo yamekuwa yakitokea, ikiwamo kuteketea wanapovamia magari ya mafuta.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Itolewe elimu 'kisawasawa' itakayofanikisha sensa 2022

Na Reubeni Lumbagala

**TAFSIRI** ya sensa kwenye kamusi ni mchakato wa kupata na kutunza habari kuhusu idadi ya watu, makazi au taasisi, aidha ni utaratibu rasmi wa mara kwa mara wa kuhesabu watu kwenye taifa. Tanzania inafanya sensa kila baada ya miaka 10 huku Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikiratibu na kusimamia jukumu hilo.

Agosti 2022, taifa linatarajia kufanya sensa ya watu na makazi ili takwimu zitakazopatikana ziwe nyenzo muhimu za kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Ikumbukwe kuwa ili kuwa na mipango shughuli na mipango yake ya kimaendeleo, ni lazima pawepo na takwimu sahihi za raia waliopo ili mipango hiyo ya kimaendeleo iweze kugusa maisha ya watu na hatimaye dhamira njema ya kuwaletea wananchi maendeleo ifanikiwe.

Ili sensa ifanikiwe kama ilivyokusudiwa, ni lazima maandalizi ya kutosha yafanyike kabla ya kuanza kwa utekelezaji na miongoni mwa jambo la msingi kufikia mafanikio ni kutoa elimu ya sensa kwa wananchi ili wawe na uelewa wa pamoja na washirikiane na maofisa na makarani wa sensa watakapofika kukusanya taarifa muhimu.

Si wananchi wote wenye uelewa kuhusu sensa, hivyo ni muhimu wakahamasishwa umuhimu wake kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Katika kikao cha uhamasishaji wananchi kushiriki sensa jijini Dodoma, Spika wa Bunge, Job Ndugai alitoa rai kwa NBS kutoa elimu ya sensa kwa wananchi ili kuifanikisha akisema:

"Jambo la sensa ni muhimu sana watu kuhesabiwa, lakini suala hili si rahisi kwa sababu yapo baadhi ya makabila kama sisi Wagogo kumuuliza mtu una wake wangapi au mifugo mingapi ni ngumu sana hivyo elimu inahitajika sana ..."

Uzoefu uliotolewa na Spika Ndugai unagusa karibu Tanzania nzima siyo wote waliotayari kusema ukweli kuhusu watoto, mapato, wenza na mali hivyo kasi ya utoaji wa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi ni muhimu.

Elimu inahitajika kwa makundi yote kabla ya kuingia kwenye zoezi la sensa ya watu na makazi ili kuondoa mawazo na imani potofu zilizopo kwa baadhi ya makabila nchini kukataa kuhesabiwa kwa madai ya kuogopa kufa au kurogwa.

Dhana hii potofu ya kuwa kuhesabu watu kunasababisha vifo vyao itaondoka miongoni mwa wananchi kama zoezi la elimu kwa umma juu ya sensa itatolewa ipasavyo.

Sambamba na hilo, wananchi waelimishwe namna sensa inavyosaidia kufanikisha mipango ya serikali iliyozingatia idadi ya wananchi wake. Naamini, wananchi wakielimishwa kuhusu uhusiano uliopo baina ya sensa na utekelezaji wa mipango ya maendeleo, wataachana na dhana potofu juu ya zoezi la sensa.

Pia, watu waelezwe raslimali fedha takriban Shilingi bilioni 215.6 zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha sensa mwakani ni lazima zilete tija na zinufaishe taifa.

Bilioni 215.6 ni fedha nyingi sana, lakini zinatumiwa katika kufanikisha sensa kutokana na umuhimu wake katika kuchagiza maendeleo ya nchi, hivyo ni vyema wananchi wakashiriki kikamilifu.

Ni vyema wananchi wakaelimishwa namna zoezi hili linavyogharimu fedha nyingi, hivyo ni vyema wakashiriki kikamilifu kuepusha hasara na kupotea fedha ambazo ni kodi za wananchi ikiwa wananchi watashindwa kutoka ushirikiano kwa maofisa na makarani wa sensa wakati wa kuhesabiwa utakapofika.

Pamoja na kazi kubwa inayofanywa na NBS kuna haja ya kuongeza kasi utoaji elimu ya sensa kwa wananchi ikizingatiwa ili malengo ya sensa yafanikiwe ni lazima ushirikiano wa wananchi katika kutoa taarifa muhimu zinazohitajika katika madodoso ya sensa uwepo.

Viongozi wa dini, wa kimila, wa serikali kuu na za mitaa, taasisi za elimu, vyombo vya habari, wote kwa pamoja wawe mstari wa mbele kuwaelimisha wananchi na mafanikio makubwa kwa maendeleo ya Tanzania.

## Wadai bado ukiukwaji haki za binadamu upo

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesema Tanzania bado inakabiliwa na ukiukwaji wa haki za binadamu hasa katika maeneo ya uhuru wa habari, vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, wakati wa mkutano wa mapitio ya hali ya haki za binadamu ulioandaliwa na mtandao huo na kukutanisha wadau mbalimbali wa maendeleo.

Olengurumwa alisema ripoti yao inaonyesha katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2017 hadi 2020 kumekuwa na ukiukwaji huo licha ya serikali kukubali baadhi ya mapendekezo 133 yaliyotolewa na watetezi wa haki za binadamu.

Alisema kukosekana kwa uhuru wa kujieleza, utungwaji wa sheria kali kwa vyombo vya habari, kuzuiwa kwa watetezi wa haki za binadamu kutekeleza majukumu yao, vyote hivyo vimesababisha kuzolota kwa haki za binadamu nchini.

Aidha, alisema yapo maeneo ambayo nchi imefanya vizuri karibia asilimia 60 ingawa bado kuna ukiukwaji wa haki za binadamu unaoendelea.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, alisema serikali imekuwa ikithamini mchango wa asasi za kiraia na kuheshimu haki za binadamu.

Alisema kwa miaka minne iliyopita mashirika hayo ya watetezi walitoa jumla ya mapendekezo 227 kati ya hayo 133 ndiyo yalikubaliwa na serikali huku mengine yalikataliwa sababu yalikuwa kinyume na sheria, mila, imani na desturi za nchi.

"Mfano kulikuwa na masuala ya ushoga tulikataa na tukawaeleza kuwa serikali itafuatali kupokea mapendekezo yatakayoendana na desturi mila na tamaduni zetu, wakiibua tena ambayo hayaendani wala hatutayatekeleza kwani huo ndio msimamo wa nchi yetu," amesema.

# Hukumu Mkurugenzi MSD Oktoba 22

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia kutoa hukumu, dhidi ya aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Cosmas Mwaifwani, na mwenzake Oktoba 22, mwaka huu.

Uamuzi huo ulifikiwa jana katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Mwaifwani na aliyekuwa Meneja Ununuzi wa MSD, Fredrick Nicolous, wanakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka na kusababisha Kampuni ya H.H Hillal kupata manufaa ya zaidi ya Sh milioni 400.

Wakili wa Serikali Janeth Kafuko akiiwakilisha Jamhuri, alidai kesi ilikuja jana, kwa ajili ya hukumu, washtakiwa wote walikuwapo, lakini mawakili wao hawakuwapo. Hakimu Simba alisema pande zote mbili ziliwasilisha hoja za mwisho za majumuisho na mpaka jana alipokea hoja hizo, hivyo atazipitia na kutoa hukumu Oktoba 22.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi 10 na upande wa utetezi washtakiwa walijitetea wenyewe.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wakidaiwa kutenda kosa hilo kati ya Machi Mosi hadi 19, 2013 katika makao makuu ya MSD, Keko, Temeke, Dar es Salaam.

Inadaiwa washtakiwa wote kwa pamoja wakiwa waajiriwa wa MSD walitumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa na kufanya mabadaliko ya mkataba namba 1, wenye kumbukumbu MSD/003/Q/G/2010/2011/60 wa Machi Mosi, 2013 na kupitisha namba mbili wenye kumbukumbu namba kama hiyo wa Machi 19, 2013. Inadaiwa kitendo hicho kilisababisha Kampuni ya H.H Hillal kupata manufaa yasiyokuwa ya halali ya Sh 482,266,000.

# Waliochanjwa Uviko-19 Pwani waongezeka

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

IDADI ya wananchi wanaopata chanjo ya Uviko-19 katika Mkoa wa Pwani imeongezeka kutokana na kampeni harakishi shirikishi iliyozinduliwa katika mkoa huo mwishoni mwa mwezi Septemba.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini Kibaha, Mratibu wa chanjo mkoa wa Pwani, Dk. Abas Hincha, alisema hadi sasa wananchi waliochanjwa wamefikia asilimia 75.

Alisema kampeni hiyo imesaidia kufikisha elimu mpaka ngazi ya chini na wananchi wanaohitaji kuchanja wanafikiwa popote walipo. Hincha alisema tangu walipopokea chanjo 30,000 mwezi Julai hadi kufikia Oktoba 4, wananchi 22,286 wa Mkoa wa Pwani wamechanja sawa na asilimia 75.

Mratibu huyo alisema kabla ya kuzindua mkakati wa kampeni hiyo mwishoni mwa mwezi Septemba utoaji wa chanjo ulikuwa umefikia asilimia 49 kwa muda wa wiki mbili ya elimu hali imebadilika.

Hincha alisema pia ongezeko la vituo vya kutolea chanjo limesaidia kwa kuwa wananchi wenye uhitaji walisogezewa huduma hiyo karibu na maeneo yao kutoka vituo 27 na sasa vimefikia 287 kwa mkoa wote. Alisema chanjo iliyobaki kwasasa ni chini ya dozi 5,000 ambayo muda mfupi ujao itakuwa imeisha kutokana na kasi ya ongezeko la wananchi kujitokeza kuchanja.

"Wiki mbili zijazo tutakuwa tumemaliza chanjo iliyopo kwa sasa watu wengi baada ya kufikiwa na elimu wamekuwa wakijitokeza katika Halmashauri ya Kibaha vituo vyote ikifika Oktoba 6 huenda kukawa hakuna tena chanjo iliyobaki kutokana na namna wananchi wanavyoendelea kujitokeza," alisema.

Alisema utaratibu wa kuwafikia wananchi walipo ikiwamo nyumba kwa nyumba na kwenye vituo kwa makundi mbalimbali yanayohitaji chanjo hiyo umekuwa moja ya sababu za ongezeko la waliochanja. Kampeni harakishi shirikishi ilizinduliwa Septemba 24 na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, huku kukiwa na asilimia 49 pekee ya wananchi waliochanja na hadi kufikia Oktoba 4 idadi imeongezeka na kufikia asilimia 75.


**Bank of India (Tanzania) Ltd.**

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

*Relationship beyond banking*

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|---|
| | | USD | TSHS |
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | **Up to** Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | **Over** Tshs 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | **Up to 5000 USD a day** | free | - |
| | **Over 5000 USD withdrawal** | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | • Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | • Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | • Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | **Deposit fee** | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.10% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| **3.0** | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| **4.0** | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
| | **-Individual** | free | free | Free |
| | **-Corporate** | free | free | Free |

| | | | |
|---|---|---|---|
| e) | Others | - | - |
| **5.0** | **Foreign Exchange Transaction.** | - | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | – |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | – |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | – |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **6.0** | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | **-Individuals** | 3 | 5,000 |
| | **-Corporate** | 6 | 12,000 |
| **7.0** | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| **8.0** | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| **9.0** | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| **10.0** | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 05.10. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 05.10. 2021 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 05.10. 2021 |

**OTHER DISCLOSURES**
**(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| **3.0** | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **4.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 5.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 05.10. 2021 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 05.10. 2021 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 05.10. 2021 |

216495102

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB Close to you

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| **1** | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| **2** | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| **3** | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| **4** | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |

| 6 | ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 5,900 ; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |

| 7 | MOBILE (SMS) BANKING | | |
|---|---|---|---|
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |

| 8 | INTERNET BANKING | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |

| 9 | MONEY REMITTANCES | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES | | |
|---|---|---|---|
| A | TYPES OF LENDING RATES | LENDING RATES - PA (%) | |
| | | TZS | USD |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

B FIXED DEPOSITS


| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Saving account rates up to 12%**

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head Retail Products & Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**




216495602

www.nmbbank.co.tz

HABARI KITAIFA

## Waziri aridhishwa hatua Coca-Cola utunzaji mazingira

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameridhishwa na kampuni ya Coca-Cola Tanzania kwa hatua yake ya kubadili mwonekano wa rangi ya chupa ya plastiki ya soda ya Sprite, ambapo mabadiliko hayo yanachangia utunzaji mazingira.

Akizindua mwonekano huo mpya wa Sprite, Waziri Jafo alisema hatua hiyo inaongeza njia kwa kutumia malighafi za vifungashio ambavyo zinaweza kutumika na kurejelezwa tena viwandani na kutengeneza bidhaa nyingine tofauti na zile zenye rangi.

"Ndugu zangu tuvumiliane itakapokuja kanuni na kuwa ngumu zaidi ukimbana mtu mwenye chupa ya rangi tuvumiliane, tunachotaka ni kwamba suala zima la mazingira yanatunzwa.

"Ndani ya miezi 12 mtaona mabadiliko makubwa katika suala zima la wale wanaotumia chupa zenye rangi, mabadiliko hayo yanakuja kwa mujibu wa sheria. Ninataka kabla mwaka haujaisha kanuni zianze kufanya kazi."

Jafo aliwataka wadau wote wakiwamo wawekezaji wakubwa wafanye mabadiliko hayo kwa vitendo kwa kuiga kilichofanywa na kampuni ya Coca-Cola.

"Chupa hizi zisizo na rangi, mwokota chupa akiikuta barabarani hata inyanyapaa, ninafahamu wapo wadau wengine wa viwanda, nimewaagiza watu wangu wawaambie mambo mawili.

"Moja, ninataka kampuni zinazotengeneza vinywaji wahakikishe wanaweka vinywaji vyao kwenye chupa isiyo na rangi ili ziweze kurejelezwa viwandani ama ikishindikana anayetoa chupa ambayo ina rangi ahakikishe kwa asilimia 100 tusizikute mtaani awe na mtambo wa kuzirejeleza mwenyewe."

Jafo aliwakumbusha kuwa mazingira hayana mbadala hivyo wana kila sababu ya kuyalinda kwa kuwa dunia inataabika na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira.

Alisema Oktoba 30 hadi Novemba 11, mwaka huu huko Scotland kutafanyika mkutano ambao ajenda kubwa ni kujadili mazingira.

"Kwa bahati mbaya chupa hizi zisiporejelezwa wengine wataamua kuzichoma moto na kwenda kuharibu hewa ukanda na madhara yake ni makubwa kwa viumbe hai, mimea na wanadamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Coca-Cola Kwanza, Tanzania Unguu Sulay, alisema wateja wao wataburudika na kinywaji chao huku chupa yake ikiweza kurejelezwa kwa urahisi na kwa kutumika tena kutengeneza bidhaa mpya.

Alisema chupa mpya isiyo na rangi itakuwa na mchango kiuchumi kwani itakuwa na thamani zaidi kwa warejelezaji wa taka Tanzania ambao wanategemea kukusanya na kuuza taka zinazotokana na vifungashio vya pastiki kwa kujiingizia kipato.

Mkurugenzi wa masuala ya Umma na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Salum Nassor, alisema mabadiliko hayo yamelenga kuunga mkono jitihada endelevu za serikali zinazoendana na sera ya mazingira na mikakati endelevu ya kitaifa.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema changamoto kubwa ni chupa zenye rangi kuzagaa maeneo mbalimbali yakiwamo ya ufukwe, maziwa, makorongo, mito na maeneo mengine.

# Mahatma Gandhi bado alama kutafuta ukombozi bila vurugu

**Na Romana Mallya**

MWASISI wa India, Mahatma Gandhi, anaendelea kumiminiwa sifa ya kupigania ukombozi bila kutumia vurugu.

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Ubalozi wa India nchini, wameshereheke a siku ya kuzaliwa kwa Mahatma Gandhi, ambaye ni Baba wa Taifa wa India.

Gandhi ni shujaa wa uhuru nchini humo ambaye alipigania ukombozi wa nchi bila kutumia vurugu.

Sherehe hizo ambazo kila mwaka huenda sambamba na siku ya kupinga vurugu na ukatili duniani, ziliadhimishwa mwishoni mwa wiki chuoni hapo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Gandhi, amekuwa msukumo kwa harakati zisizo za vurugu za haki za raia na mabadiliko ya kijamii ulimwenguni.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, aliangazia umuhimu wake katika muktadha wa ulimwengu wa sasa na kusema:

"Ni Afrika iliyombadilisha mwanasheria Gandhi kuwa Mahatma (roho ya kipekee). Miaka 21 aliyoishi Afrika Kusini ilikuwa na nafasi kubwa katika mageuzi ya mtazamo wa Mahtma Gandhi kisiasa na namna alivyoonyesha kuguswa na hali halisi na uzoefu ambao uliwavutia viongozi wa Afrika akiwamo Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na Baba wa Taifa la Afrika Kusini, Nelson Mandela, namna Gandhi alivyokuwa kiungo muhimu kati ya India na nchi za Afrika."

Balozi huyo alielezea namna Gandhi alivyoliunganisha taifa hilo kiuhusiano na nchi nyingine za Afrika ikiwamo Tanzania, na kwamba kwa kufuata mafundisho yake, India imekuwa ikihakikisha kunakuwa na maendeleo katika nchi za Asia na Afrika.

Alisema kila mwaka ubalozi huo umekuwa ukidhamini mafunzo ya elimu ya juu kwa kuwapeleka mamia ya vijana wa Watanzania India kupitia programu mbalimbali wanazozitoa.

Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangamalle, alisema Mahatma ndiye mtu aliyeudhihirishia ulimwengu kwamba njia ya amani na ya bila matumizi ya vurugu ndiyo yenye ufanisi na ya kudumu katika kuushinda udhalimu.

"Ni mtu aliyetoa msukumo jumuishi wa kanuni za uvumilivu na amani," alisema.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wapili kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto), wakiwa katika kikao na Wajumbe wa Bodi ya Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi (ATOGS), jijini Dodoma jana. Wapili kulia ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Abdulsamad Abdulrahim. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamba: Tuko tayari kufanyakazi na ATOGS

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, ameeleza kuwa, Wizara ya Nishati iko tayari kufanya kazi na Jumuiya ya Watoa Huduma katika Sekta ya Mafuta na Gesi (ATOGS) ili kuendelea kuwezesha wananchi kushiriki ipasavyo katika sekta hiyo.

Makamba alisema hayo juzi alipofanya mazungumzo na Wajumbe wa Bodi hiyo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Abdulsamad Abdulrahim, baada ya Jumuiya hiyo kufika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma kwa ajili ya kueleza malengo yake na masuala mengine yanayohusu jumuiya hiyo ambayo ina wanachama takribani 128.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato; Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja; Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ( TPDC), Dk. James Mataragio na Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ( PURA), Charles Sangweni.

"Sisi tuko tayari kufanya kazi na ninyi, kwani tunaamini wananchi wengi wanaweza kunufaika na fursa zinazotokana na hii sekta kutokana na uwepo wa jumuiya hii ambayo inawapa wananchi taarifa mbalimbali kuhusu fursa zilizopo pamoja na kuwaunganisha na mamlaka mbalimbali pamoja na wafanya maamuzi," alisema Waziri Makamba.

Alisisitiza kuwa Wizara ya Nishati na taasisi zake zitaunga mkono taasisi au jumuiya ambazo zina malengo chanya ikiwamo ya kuwaunganisha wananchi na kuwapa fursa na taarifa zitakazowasaidia katika kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Wajumbe wa jumuiya hiyo waliushukuru uongozi wa Wizara ya Nishati kwa kuwapokea na kuwasikiliza na kueleza kuwa nia yao ni kushirikiana na serikali katika utaratibu wowote utakaopelekea wananchi wengi washiriki kwenye shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Mafuta na Gesi.

# Wanaume wapewa jukumu saratani mlango wa kizazi

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

WANAUME mkoani Kagera wametakiwa kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele katika kuwahimiza wenzi wao kufanya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizindua mradi wa uhamasishaji wanawake hasa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kupima saratani ya mlango wa kizazi wilayani humo.

Mradi huo unatekelezwa na Shirika lisilokuwa la Kiserikali linalosaidia Wanawake waishio na Virusi Vya UKIMWI Mkoa wa Kagera (AMWAVU) kwa kuratibiwa na TACAIDS na kufadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia uwezeshaji wa Wanawake, (UN-WOMEN).

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Machali alisema ni muhimu kwa wanaume kuwahimiza wenza wao kwenda kutazama afya zao kwa kufanya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi.

"Sisi wanaume pamoja na wake zetu tunao wajibu wa kuihamasisha jamii kuitikia kwenda kufanya uchunguzi ili tuweze kulitokomeza tatizo hili. Nawaasa wanaume wawashauri wake zao kwenda kupima ugonjwa huu ambao unagharimu maisha yao bila ulazima."

"Kama kuna wanaume ambao wanaozuia wake zao kwenda kupima waache tabia hiyo mara moja badala yake wawasukume waende wakapime tena wawe wakali pale ambapo wake zao hawataki kuelewa na kwenda kufanya uchunguzi kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewasaidia akina mama na sisi tutaishi maisha yenye furaha sababu hapatakuwa na mgonjwa ndani yake,"alisema.

Aliongeza: "Hivyo ni wajibu wa kila mwanaume kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa familia inakuwa na uhakika wa afya, hivyo ni wajibu wa kila mwanaume kuhimiza mwenza wake katika hili ili kujihakikishia usalama wa afya."

Hata hivyo, alisema wanaume kazi yao kubwa ni kuhakikisha kuwa wanawake wanapima na kwamba iwapo wao wataweka mkazo basi itakuwa rahisi.

"Bahati nzuri tuna vituo vinavyotoa huduma bila malipo, wanaume kazi yetu kubwa ni kuhakikisha wake zetu wanapima kwani mara nyingi wanawake wakipeleka wazo nyumbani huwa halina uzito tofauti na baba ambapo akipeleka linakuwa na uzito na linafanyiwa kazi kwa haraka," alisema. Kwa upande wake, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Safina Yuma, alisema kuwa ni busara kwa wnaume kuhimiza wenza wao kufanya uchunguzi.

"Saratani kuna wanaume ambao wanaweza kuwaelimisha wenza wao na wakaenda kupima, hivyo ni jukumu la mwanaume pia katika kuhakikisha kuwa afya ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi inapewa kipaumbele katika familia hatua itakayosaidia kufikia lengo la kuutokomeza ugonjwa huu," alisema.

Naye, Mkurugenzi wa Habari na Uraghibishi kutoka TACAIDS, Jumanne Issango, alisema kuwa uhusika wa wanaume ni muhimu katika kufanikisha lengo hilo.

"Uhusika wa wanaume ni kitu muhimu sana, hivyo pamoja na kuwahimiza wanawake kufika kwenye vituo vya uchunguzi, bado ni muhimu pia kwa wanaume kushirikiana bega kwa bega na wenza wao wanawake ili kusaidia kufikia lengo la kutokomeza ugonjwa huu ifikapo 2030," alisema Issango.



Meneja wa Benki ya Azania tawi la Lumumba, Valentina Chasamba (katikati), akikabidhi vitanda kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Azania, Melisius Kayombo (kulia), vilivyotolewa na benki kama sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mkenda atambua mchango TADB kwenye kahawa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, ameridhishwa na jitihada za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuendelea kutoa mchango wake kwa maendeleo and ukuaji wa zao la kahawa nchini.

"Ninatambua mchango wa TADB kwa maendeleo na ustawi wa zao la kahawa nchini na ushiriki wenu kwenye Maonyesho ya Kahawa Mwaka 2021 yanayofanyika hapa mjini Moshi ni kielelezo tosha cha dhamira yenu," alisema Waziri Mkenda.

Benki ya TADB imetoa Sh. bilioni 130.81 kwenye zao la kahawa kwa wakulima nchini, ambayo inajumuisha viatilifu, mashine za kahawa, mbolea, vituo vya CPU, ujenzi wa maghala, na uoteshaji wa miche Ngara.

Akizindua Tamasha la Kahawa sambamba na kusherekea Siku ya Kahawa Dunia zinazosherekewa kitaifa mkoani Kilimanjaro, Waziri Mkenda alisema: "Nimeona mambo mengi katika maonyesho haya ikiwamo, miche bora, ufungaji wa kahawa umekua mzuri sana, na nashukuru benki zetu hususani TADB kwa kudhamini na kushiriki tamasha hili na muendelee kuwagusa wakulima wa kahawa moja kwa moja."

Waziri Mkenda alisema Tanzania kwa Afrika Mashariki ndio nchi pekee tunaozalisha kahawa ya papo hapo (Instant Coffee), hivyo kuna kaza kubwa yakuendelea kuitangaza kahawa ya Tanzania ili kufungua masoko zaidi Afrika."

"Nimeongea na TADB na wameonyesha utayari wa kutoa fedha kwa wakulima ili kubadilisha miche yao yenye tija kubwa kuongeza uzalishaji wa kahawa nchini," alisema Prof. Mkenda.

Afisa Mwandamizi wa Maendeleo ya Biashara, Zakayo Mphuru, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Frank Nyabundege, alisema ushiriki wa TADB kweye maonyesho ni kutambua mchango wa mnyororo wa thamani wa zao la kahawa nchini.

"Tunashiriki haya maonyesho ya siku ya kahawa duniani kwa sababu TADB imekuwa mdau mkubwa wa mnyororo mzima wa thamani wa zao la kahawa na kimsingi TADB imehusika moja kwa moja kuwezesha sekta hii kukua kwa kuwafikia zaidi ya wakulima wanufaika 150,000 wa zao la kahawa," alisema.

# Mpango kutoa tuzo mzalishaji bora wa mwaka

**Na Joseph Mwendapole**

TUZO za Rais kwa Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA), zitatolewa Ijumaa wiki hii na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Leodgar Tenga, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tuzo hizo kwa mwaka 2020.

Mdhamini mkuu wa tuzo hizo kwa mwaka huu ni benki ya CRDB, wengine ni ITV/Radio One, Tanga Cement, ALAF Limited Motisun Group, GIZ Business Scouts for Development, TRA na Serena.

Tenga alisema PMAYA ni tukio kubwa la mwaka la kutambua nafasi ya wenye viwanda kwenye ukuaji wa sekta ya uchumi na wadau mbalimbali wanakutana na kubadilishana mawazo kuhusu maendeleo ya sekta hiyo.

Alisema jumla ya viwanda 78 vimeshindanishwa na vilivyokidhi vigezo na kushinda tuzo kwenye sekta mbalimbali vitapewa tuzo zao Ijumaa kwenye tukio ambalo litakutanisha wadau wa sekta mbalimbali za uzalishaji.

"Hizi ni tuzo za Rais na yeye ndiye anatoa tuzo, lakini tunashukuru safari hii ameamua kutupa Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango amwakilishe, wazalishaji wamefurahi sana na wanamsubiri kwa hamu siku ya Ijumaa," alisema Tenga.

Aidha, Tenga aliishukuru kampuni ya DataWorks Associate Limited ambayo ndiyo ilifanya tathmini kupitia vigezo mbalimbali vilivyowekwa kwenye ushindani ili kuwapata washindi na hatimaye kuwapata.

Akizungumza kwa niaba ya ITV/Radio One, ambayo ni miongoni mwa wadhamini wa tuzo hizo, Deogratius Rweyunga, alisema kituo hicho kinajisikia fahari kuwa miongoni mwa wadhamini wa tukio kubwa kama hilo ambalo linawakutanisha wenye viwanda.

Alisema aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Hayati Reginald Mengi, alitoa mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya viwanda nchini hivyo kituo hicho hakina sababu yoyote ya kuacha kuunga mkono sekta ya viwanda.

"ITV na Radio One inaona fahari kuwa miongoni mwa wadhamini wakubwa wa tukio hili na kwasababu Mwenyekiti wetu alikuwa mstari wa mbele kukuza sekta hii sisi hatuwezi kuwa na sababu yoyote ya kujiweka pembeni na tunaahidi kuendelea kushirikiana na CTI," alisema.

Mkurugenzi wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, aliipongeza CTI kwa kuandaa tuzo hizo ambazo alisema zimekuwa zikileta chachu kubwa kwenye maendeleo ya viwanda nchini.

"Sisi tumekuwa wadhamini wakuu wa PMAYA kwa miaka mitatu mfululizo na tuna kila sababu ya kufanya hivyo kwasababu ni kupitia tuzo kama hizi wenye viwanda wanahamasika kuzalisha bidhaa bora zinazokuwa na ushindani kwenye soko," alisema Nsekela.



Ukurasa 12

Harakati za 50/50 wanawake sasa kuzifikisha mitandaoni



Ukurasa 13

Makamu wa Pili wa Rais SMZ anapoibua wajibu wa wanaCCM uchaguzi 2025


# siasa

JUMATANO OKTOBA 6, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

## Watuhumiwa uhalifu wa binadamu wanaotamba na nishani za Nobel

# Mwanaharakati: Rahisi kwa mama kushika uongozi juu, kuliko chini

Na Christina Mwakangale

WAKATI lengo la kuwa na usawa wa kijinsia katika uongozi maarufu 50/50, linalowapa nafasi sawa ya uongozi wanawake na wanaume ifikapo mwaka 2030, vipo viashiria vinavyouweka mashakani uwezekano wa kufikia hapo, kutokana na hali ya wanawake kubinywa kwenye nafasi za uongozi kuzidi kuota mizizi hasa kwenye mashina.

Takwimu za madiwani kitaifa zinadhihirisha vikwazo hivyo, anasema Deogratius Temba, na kuongeza kuwa, asilimia tano ya madiwani wote nchini ni wanawake na waliobaki 95 ni wanaume.

"Ni rahisi kupata mbunge au rais mwanamke kuliko kumchagua mwenyekiti wa mtaa au kijiji. Huko chini mwanamke kuaminiwa na kupenya katika uongozi ni kazi kubwa kuliko ilivyo juu, sababu mojawapo ni dhana za kijinsia, mila na desturi potofu," anasema Temba.

Temba mwezeshaji katika mafunzo ya uwezeshaji wanawake yaliyofanyika Dar es Salaam, hivi karibuni na kushirikisha wadau wa usawa wa kijinsia, wanaharakati, madiwani, watendaji wa kata na wenyeviti wa serikali za mitaa. Hoja ya vikwazo vinavyowakwamisha wanawake kwenye uongozi ikaibuka kila wakati.

"Kwenye mikoa 15 ambayo tumeifikia na kutoa elimu kuhusu masuala haya tumebaini kuna ugumu wa hali ya juu wanawake wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya chini kwenye mashina, vitongoji, vijiji na kata kupewa fursa."



Baadhi ya viongozi wa Kata za Saranga na Mabwepande Dar es Salaam, wakishiriki mafunzo kuhamasisha kufikia usawa wa kijinsia. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Anataja dhana zinazowakwamisha kuwa ni mfumo dume, mawazo mgando na mgawanyo wa majukumu ya kijinsia kwenye jamii inayosababisha baadhi ya jamii kuamini kwamba kazi ya uongozi ni kwa wanaume pekee.

"Maeneo tunakofanyia kazi wanawake wenyeviti wa mitaa ni wachache na kwingine hakuna kabisa, kuliko na nafuu ni mkoani Morogoro ambako kuliwahi kuwa na mwenyekiti wa halmashauri. Asilimia tano ya madiwani Tanzania ni wanawake na waliobaki wote ni wanaume," anasema Temba.

Rais Samia suluhu Hassan, mara kadhaa amezungumzia suala la uongozi kwa kuzingatia usawa kijinsia na amelionyesha hilo kwenye uteuzi unaoongeza idadi ya wanawake kwenye maeneo mbalimbali mfano majaji, mabalozi, mawaziri, bungeni mikoa na halmashauri za wilaya akilenga kufikia lengo la 50/50.

Hata hivyo, juhudi za kuwapaisha wanawake kwenye uongozi kuanzia mashinani, mitaani na vijijini zinakwamishwa na vikwazo vinavyotokana na dhana zilizopo kwenye jamii, mifumo, utamaduni na sera, kwa mujibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Mawazo mbadala ni muhimu ili kusaidia kuwaweka watu kwenye mstari. Mila na desturi katika eneo fulani zinasababisha kuwapo mawazo mgando kwamba kazi hii ni ya mwanamke, au ya wanaume, wenzetu nchi zilizoendelea wamepiga hatua kwa sababu ya viongozi kuwa shirikishi watu wa makundi yote."

Mwezeshaji huyo anaongeza kuwa baadhi ya maeneo watu wanadhani haiwezekani mwanamke kuwa dereva, na kwamba kuna madhara ya kimaendeleo kutokana na mfumo dume, mawazo mgando, sera, sheria kandamizi ambazo taifa limejiwekea .

### UBUNGO YACHEMKA

Diwani wa Viti Maalum Liberata Samson , anasema Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam ina madiwani wanawake sita katiya 19 huku wenyeviti wa mitaa wakiwa wanne na waliobakia 90 ni wanaume.

Aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Diwani wa Kata ya Ngerengere, Kibena Nassoro, anasema mkakati wa wanawake ni kwamba ifikapo 2025, idadi ya wenyeviti kwenye halmashauri hiyo iongezeke.

Kibena ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Wanawake Viongozi Serikali za Mitaa (WASEMI), anasema wataendelea kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea na kushinda, bila kukata tamaa.

"Mimi ni miongoni mwa wanawake watano wenyeviti wa halmashauri nchini, kati halmashauri takribani 180, hapa mtaona bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunafika ngazi za maamuzi hususan wenyeviti wa halmashauri, ili kuhimiza masuala ya kijinsia kwenye jamii," anasema Kibena.

### MIKATABA KIMATAIFA

Abbas Mwalimu, mchambuzi wa masuala ya kisiasa anasema mkataba wa kimataifa unaopinga aina zote za ukandamizaji dhidi ya wanawake (CEDAW), unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua maalumu zisizo za kudumu kama kuwateua wabunge wa viti maalum ili kuleta usawa baina ya wanawake na wanaume.

Anasema ana imani na wanawake kuwa wanaweza kuleta mabadiliko chanya katika vyombo vya maamuzi wakiwezeshwa na wakijiwezesha. Rais Samia Suluhu Hassan ni mfano wa namna wanawake na kinamama wanavyoweza kuleta matokeo chanya na makubwa katika nchi.

Anashauri kujenga mifumo imara ya kuwapata wale watakaoweza kuvaa viatu vya wale watakaomaliza muda wao kisheria na kwa mujibu wa katiba na kuongeza: "Lakini pia kuna haja ya kurejea tafsiri hii ya 'hatua maalumu zisizo za kudumu' ili kuwapo na utaratibu wa kuachiana madaraka na uongozi ulio bora, hasa ikihusisha wanawake vijana katika uongozi. Nadhani hapa ile tafsiri waliyolenga Umoja wa Mataifa kupitia CEDAW inaweza kuleta usawa na hatimaye kufikia malengo endelevu ya milenia (SDGs)."

# Harakati za 50/50 wanawake sasa kuzifikisha mitandaoni

**Na Yasmine Protace**

MJADALA kuhusu wanawake na uongozi, wenye jina 'kilinge cha simulizi' ukikutanisha kinamama kutoka taasisi mbalimbali za kiraia na vyama vya siasa, unachanja mbuga kutekeleza ajenda ya kushirikisha watu wengi zaidi kudai usawa wa kijinsia kwa kupitia mitandao.

Kilinge hicho cha simulizi, mjadala wake ulifanyika Dar es Salaam, harakati za uongozi na masuala ya kijinsia kupitia mitandao ya kijamii, ndiyo iliyokuwa sehemu kubwa ya mazungumzo yake, ukishirikisha vijana na wazee, waliojadili jinsi ya kutumia mitandao hiyo kupitisha ajenda hiyo kuu.

Mwezeshaji wa mjadala huo, Sadaka Gandi anasema, ajenda kuu ya wanawake na vijana, ni usawa wa kijinsia na kwamba umefika wakati kuifikisha kwa watu wengi zaidi, kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano.

Anafafanua kuwa watu hawasomi vitabu, wanatumia zaidi mitandao ya kijamii, hivyo wanawake waitumie kupenyeza ajenda yao, akiamini kwamba ni rahisi taarifa hizo kufikia wengi na kujulikana.

"Katika kilinge cha simulizi, tunataka tukubaliane kwa pamoja kwamba umefika wakati sasa sisi wote bila kujali umri wetu, tutumie mitandao ya kijamii kufikisha ajenda yetu kwa watu wengi zaidi," anasema Gandi.

Anawaeleza washiriki kuwa wanawake wana uwezo wa kuongoza kama walivyo wanaume, na kwamba kinachohitajika ni utashi wa kisiasa kusaidia kuongeza kikamilifu na kwa makusudi uwakilishi wa wanawake.

"Tunahitaji kutumia mitandao ya kijamii ili ajenda yetu ifike mbali zaidi, lakini tunaweza kuitumia kuweka historia za wanawake wanaharakati wa Tanzania ambao wamechangia katika ukombozi wa nchi hii," anasema.

**ATAJA KINACHOKWAMISHA**

Hata hivyo, katika mjadala huo, inaibuka hoja kuwa wapo baadhi ya wanawake hawatumii mitandao hiyo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa elimu sahihi ya jinsi ya kuitumia.

Meneja Mafunzo kutoka Taasisi ya Reach and Save the Needy (RESANE), Neema Komba, anasema, wanawake watu wazima hawajui kutumia mitandao hiyo na kwamba ipo haja ya kuwaelimisha.

"Baadhi yao wanadhani mitandao hiyo ni uhuni au ni kwa ajili ya vijana pekee, lakini ukweli ni kwamba sote tunapaswa kuitumia kwa mambo mengi ikiwamo harakati za kutafuta usawa za kijinsia," anasema Neema.

Adelina Muluge kutoka Sauti ya Wanawake Wenye Ulemavu (SWAUTA), anasema, wanawake hasa walio kwenye ndoa, hawako huru kutumia mitandao hiyo, kwa maelezo kuwa wanazuiliwa na waume zao.



Kilinge cha simulizi kikiendelea chini ya mwezeshaji Sadaka Gandi. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

> Tunahitaji kutumia mitandao ya kijamii ili ajenda yetu ifike mbali zaidi, lakini tunaweza kuitumia kuweka historia za wanawake wanaharakati wa Tanzania ambao wamechangia katika ukombozi wa nchi hii.



Baadhi ya washiriki wa kilinge hicho.

Anasema kwa mazingira hayo, inawawia vigumu kutoa mchango kwa mambo yanayohusu harakati za kumwezesha mwanamke kupata uongozi kama ilivyo kwa wanaume.

"Mwanaume anakuzuia kutumia simu au anakuchunguza hali inayo inakwamisha wanawake wengi kushiriki kikamilifu kwenye harakati hizo ambazo tunazijadili hapa leo," anasema Adelina.

Anataja kikwazo kingine kuwa ni majukumu mengi ya nyumbani ambayo kwa namna moja au nyingine yanamfanya mwanamke kukosa muda wa kuingia kwenye mitandao ya kijamii kujua kinachoendelea duniani.

**KUACHA HOFU**

Zawadi Mkweru kutoka Jamii Forum, anawataka wanawake watu wazima kutumia mitandao hiyo kama wanavyofanya vijana, kwa kuwa inawaunganisha kwa pamoja ili kujadili mambo yanayowahusu.

"Mimi ni kijana, sikubaliani na mawazo kwamba kutumia mitandao ya kijamii ni uhuni au hatari, bali hayo yanaweza kutokea kulingana na jinsi wewe mwenyewe unavyoitumia," anasema Zawadi.

Anakiri kwamba, wapo baadhi ya vijana wanaoitumia mitandao hiyo vibaya kutokana na ukosefu wa elimu sahihi, lakini anashauri washiriki wa mjadala huo kwenda kwenye maeneo yao kutoa elimu sahihi.

"Hapa tupo vijana na watu wazima kutoka taasisi mbalimbali na pia katika vyama vya siasa, hebu sisi wenyewe tuwe chachu ya kuleta mabadiliko katika matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii," anasema.

Zawadi anahimiza kutoa elimu ikiamini itasaidia vijana kujua matumizi sahihi na pia watu wazima nao ambao wanajiweka pembeni watakuwa tayari kuitumia mitandao ili kufanikisha harakati wanazozitaka.

Angella Karashani kutoka Taasisi ya LP Digital, anasema mjadala huo wa kilinge cha simulizi ungefaa kuwa mwanzo wa mabadiliko kwa kila mmoja kutambua kuwa siku hizi kila kitu kinakwenda kwa njia ya mtandao.

"Tunajadili uongozi na masuala ya kijinsia kwenye mitandao, hii ni fursa nzuri ya kuhakikisha dunia inajua jinsi wanawake wanavyofanya harakati za kutafuta usawa wa kijinsia, hivyo tusiwe nyuma kuitumia," anasema Angella.

**KUUNGANISHA NGUVU**

Katika hitimisho la mjadala huo, wanasema kuwa sasa umefika wakati wa kuungana kati ya wanawake watu wazima na vijana, ili waelimishane kuhusu umuhimu wa kutumia mitandao katika harakati zao.

Joyce Mkina ambaye ni kiongozi wa Idara ya Nguvu ya Pamoja kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania waliokuwa waratibu wa mjadala huo wa kilinge cha simulizi, anasema kuna haja kuunganisha makundi hayo.

"Kila upande ukubali udhaifu kwanza na kisha tuanzishe muungano wa kupigania haki za wanawake kupitia mitandaoni kwa kushirikisha vijana wa sasa na wa zamani, ili ajenda yetu iende mbali zaidi," anasema Joyce.

Anawasisitiza washiriki kufahamu kuwa katika harakati hizo, hakuna kundi linaloweza kusimama bila kushirikiana na jingine, huku akisisitiza kuwa uwepo wa mwanamke katika majukwaa ya kidigitali kwenye masual ya uongozi ni muhimu.

"Na mimi ninaongezea kuwa dhana kwamba, mitandao ya kijamii haifai na siyo sehemu ya mtu mwenye heshima, isipewe nafasi, bali inategemea ni jinsi gani mtu wenyewe anavyoitumia," anasema.

Anaongeza kuwa, kwenye mitandao ya kijamii, mtu anaweza kupata historia za wanaharakati, kama Lucy Lameck, Bibi Titi Mohamed, Sofia Kawawa, Mama Maria Nyerere , mawaziri wa zamana kinamama kama Tabitha Siwale na Julie Maning na kwamba jambo la msingi ni washiriki wa mdahalo huo kufikisha ujumbe kwa wengine ili kuwa katika jukwaa la kidigitali.

"Siyo kwamba hakuna juhudi zozote ambazo zimefanyika za wanawake kupata uongozi, tunaamini kwamba bado ipo haja ya kuongeza kasi hiyo ili kufikia malengo ya usawa wa kijinsia," anasema.

Anasema, viongozi wanaweza kusaidia kufikia malengo hayo kupitia uteuzi wa nafasi zote kuanzia ngazi za chini hadi juu, kwa kuwa uongozi si mzigo wa kubeba bali ni uwezo wa kuongoza na kuonyesha njia sahihi.

"Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 5(1) mtu yeyote bila kujali jinsia (mwanaume au mwanamke) mwenye umri usiopungua miaka 18 ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi," anasema ibara hiyo.

# Makamu wa Pili anapoibua wajibu wa wana CCM uchaguzi mkuu 2025

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

ZIARA ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Tanga, imeibua chachu na hamasa mpya ya kutekeleza ilani ya chama hicho mkoani Tanga.

Mlezi wa CCM akihudumia mkoa wa Tanga, anafanya ziara kuanzia Septemba 22 hadi 26 na kufika maeneo kadhaa ikiwamo Tanga Mjini, Kilindi, Handeni, Korogwe, Muheza.

Moja ya ajenda kubwa alizosafiri na kuufikishia umma ni kuwaasa wana-CCM wajiepushe na siasa za makundi na majungu miongoni mwao, badala yake wasimamie ukweli, umoja na mshikamano ili kujenga mizizi ya kuendelea kubaki madarakani.

Anasema mshikamano thabiti miongoni mwao ni moja ya nyenzo zitakazokiimarisha chama hicho, na zaidi kukifikisha kwenye uchaguzi mbalimbali ukiwamo uchaguzi mkuu wa 2025 na kuibuka ushindi wa kishindo.

Makamu wa Rais, anatoa mfano kuwa katika uchaguzi mkuu wa 2020, CCM ilipata ushindi wa asilimia 89 na hivyo kuwaasa wanachama wake kuudhibiti ushindi huo ili usiwaponyoke.

"Ushindi wa asilimia 89 tulioupata katika Uchaguzi Mkuu wa 2020 ni wetu, tunao mikononi mwetu hivyo tunapaswa kuudhibiti ili usije ukatutoka," anasema Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Pia Abdulla anasema kazi iliyopo kwa wana-CCM kuelekea 2025 ni kuhakikisha ushindi wa asilimia 11 zilizochukuliwa na vyama vingine vya siasa zinarejee CCM na kukifanya chama kuwa mshindi wa kishindo.

Awabana watumishi na kuhimiza usalama na amani pale anaposema, ili kudhibiti ushindi na kuhakikisha chama kinatwaa asilimia 11 zilizosalia, watumishi na watendaji serikalini wanapaswa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama hicho, ili kuharakisha maendeleo na ustawi wa watu katika ngazi zote kwenye jamii.

Mlezi wa CCM mkoa wa Tanga anasema pamoja na utendaji kazi wenye tija na ufanisi, ipo haja kwa Watanzania kusimama ili nchi iendelee kubaki katika misingi yenye kuchochea usalama, amani, utulivu na mshikamano.

### DUA KWA SAMIA

Abdulla anasema uongozi madhubuti wa awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kielelezo cha nchi ilivyooneemeshwa viongozi wenye sifa na maono, hivyo akawasihi Watanzania kuendelea kumwombea.

"Kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake, tunachopaswa kukifanya ni kuwaunga mkono viongozi wetu, kuwapa moyo na kuwaombea zaidi kwa Mwenyezi Mungu," anasema.

Aidha, Makamu wa Rais, anawaonya viongozi na watendaji serikalini wenye hulka ya kujihusisha ama kupanga njama dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za umma, kuacha kwa vile hayo yanakwamisha maendeleo.

Mlezi huyo wa CCM mkoa wa Tanga anasema katika kuhakikisha 'mambo hayaharibiki', ipo haja ya kufanyika kwa ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi ikiwamo kupitia kamati za siasa na viongozi wengine wa CCM.

"Ipo haja ya kuwasimamia kikamilifu watendaji wakiwamo wakurugenzi na viongozi wa CCM kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ili kujiridhisha kama ubora wake unalingana na fedha zinazolipwa," anasema.

### KUSHIRIKI SENSA

Anahimiza kuwa kuelekea kufanya sensa ya idadi ya watu na makazi ifikapo Agosti mwakani, wananchi kujiandaa na kushiriki wakati wa utekelezaji kwani ni njia mojawapo inayowezesha kupatikana takwimu zinazoisaidia serikali kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ anasema madhara yanayotokana na maambukizi ya virusi vya COVID-19 ni makubwa na yanayoziathiri familia na mataifa na kuwahimiza watu kujitokeza kuchanjwa.

Anasema wapo wanaotoa taarifa zisizo sahihi kuhusu chanjo hiyo, pasipo kutambua kwamba upotoshaji wao unaibua hasara kubwa zinazotokana na gharama za matibabu na vifo.

"Sisi viongozi wenu tumechanjwa...hata mimi nimechanjwa, ninawasihi sana ndugu zangu wa Tanga, twendeni tukachanje, tusikae kusikiliza maneno yasiyokuwa ya ukweli, chanjo hii ni kwa ajili yetu," anahimiza.

### ATOA ONYO

Mlezi huyo wa CCM katika mkoa wa Tanga anaonya dhidi ya makundi ya wanachama wa chama hicho wanajipanga kuunda safu kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025, wakianzia na uchaguzi ndani ya chama mwakani.

"Wenye azma hiyo ninawatahadharisha waache, wasidhani kwamba hawatajulikana. Chama hiki ni kikubwa, kinasikia sana na kinaona sana hivyo utajulikana tu na kujiumiza mapema," anasema Abdulla.

Anasema makundi ndani ya CCM yanachochewa pia na kiu ya 'kila mtu' kutaka kupata uongozi ama fursa zilizo chache, jambo ambalo haliwezekani.

"Siyo rahisi kila mtu akapata fursa ndani ya CCM, haiwezekani...ninawasihi sana tuyavunje makundi kama yapo yanayoundwa, tusafishe roho zetu na kuwaunga mkono wachape kazi," anasema.

Hatua ya kukabidhiwa kwake kuwa mlezi wa CCM mkoa wa Tanga, ni yenye thamani inayomfanya awiwe kuwafikisha katika uchaguzi mkuu pasipo 'makandokando'.

Mlezi huyo anasema, " yeyote anayekwenda kinyume cha katiba, kanuni, taratibu na utamaduni wa CCM, huyo anakionea chama chetu na kumwachia siyo jambo la haki," akisisitiza umuhimu wa wana CCM kujikita katika kuimarisha matawi ya chama hicho, ili kizidi kuwa na nguvu zaidi na kwa muda mrefu ujao.

> "Siyo rahisi kila mtu akapata fursa ndani ya CCM, haiwezekani...ninawasihi sana tuyavunje makundi kama yapo yanayoundwa, tusafishe roho zetu na kuwaunga mkono wachape kazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Handeni Mji, Mussa Mkombati anasema serikali ya Rais Samia, imewezesha kupatikana fedha kwa ajili ya kusukuma mbele miradi ya maendeleo mkoani Tanga.

Kwa mujibu wa Mkombati, miongoni mwa fedha zilizotolewa kwenye halmashauri hiyo ni bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Kwenkambala, milioni 248 kujenga bwawa lililopo kata ya Malezi litakalohudumia wakazi wa mitaa mitano iliyopo eneo hilo.

Aidha, Mkombati anasema katika sekta hiyo ya maji, kata ya Mabanda imepata mradi wenye thamani ya Shilingi milioni 671 ikiwa ni matokeo ya ziara ya hivi karibuni wilayani Handeni ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na kwamba visima virefu 15 vimeshatengewa bajeti na vitaanza kuchimbwa.

Kwa upande wa upatikanaji dawa, Mkombati anasema halmashauri hiyo imepokea Shilingi milioni 148 ikiwa ni sehemu ya bajeti ya milioni 258 zilizohitajika katika kipindi cha mwaka wa fedha.



Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na wananchi. **PICHA: MTANDAO**

JUKWAA LA VIONGOZI

ABIY AHMED, AUNG SAN SUU KYI

# Watuhumiwa uhalifu wa binadamu wanaotamba na nishani za Nobel

Na Ani Jozeni

UTOAJI wa Nishani ya Amani ya Nobel, mara kwa mara umekuwa ukigubikwa na utata kutokana na pengine kukosekana kwa watu wenye sifa mujarabu wanaostahili kupokea tuzo hiyo na wenye mchango halisi katika kufikia na kuleta amani.

Nishani ya Nobel hutolewa kwa yeyote aliyefanya mambo makubwa na yenye mchango wa hali ya juu na mafanikio muhimu kuboresha maisha ya binadamu. Kwa mfano wagunduzi wa masuala ya sayansi, kutetea haki na masuala ya kitaaluma.

Hata hivyo utoaji wa tuzo hiyo miongoni mwa wanasiasa watetezi wa amani unaibua utata unaotokea kwa sababu mara nyingine mambo mema waliyofanya hugeuka na waliotunukiwa wakaanza kulaumiwa pamoja na kuwekwa kwenye kundi la wanaokiuka haki za binadamu.

Kwa mfano Aung San Suu Kyi , mwaka 1991 alitunukiwa Nishani ya Amani ya Nobel alikuwa kifungoni akiteseka na kunyanyaswa na Jeshi la Myanmar au Burma. Aliishi kizuizini akitengwa na familia yake miaka kadhaa kutokana na ujasiri wa kutetea demokrasia nchi humo na dunia nzima iliomba serikali ya Burma imwachie.

Mwaka 2010 aliachiwa huru kutoka kwenye kifungo cha nyumbani na kushinda uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka 2015, alikuwa mtetezi mkuu wa haki na wakati Jeshi la Myanmar lilipoanza kuwapiga na kuwaondoa raia wake wenye jamii ya Rohingya ambao ni Waislamu wachache katika nchi hiyo yenye wafuasi wengi wa imani ya Kibudha mwaka 2017, Suu Kyi, aliyekuwa kiongozi wa serikalini ambaye aliitetea hatua hiyo.

Kundi lenye silaha linalotokana na jamii hiyo ya Warohingya, lilidaiwa kuchoma moto vituo takribani 20 vya Polisi na Jeshi likaibuka kuwaondoa wakati huo Umoja wa Mataifa, ukielezea kitendo hicho kuwa ni mauaji ya kimbari baada ya idadi ya jamii hiyo kulazimika kutoroka kuepuka kifo na kukimbia nchi yao.

Aliyelaumiwa wa kwanza katika suala hilo ni Aung San Suu Kyi, aliyekuwa kiongozi wa juu serikalini, mama huyo aliunga mkono hatua hiyo licha ya kuonekana nguzo ya kutetea haki hadi akatunukiwa Nishani ya Amanii ya Nobel.

Kisa kama hicho kinajirudia, Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, alitunukiwa nishani hiyo mwaka 2019, mwaka mmoja baada ya kuingia madarakani, alipofikia amani na Eritrea na kuendeleza mageuzi mengine ya kidemokrasia nchini humo ikiwamo kupanua madaraka ya serikali za majimbo.

Jitihada za kuweka Ethiopia katika mwelekeo wa kidemokrasia zilitumbukia nyongo wakati chama tawala jimbo la Tigray kaskazini ya nchi hiyo, ambao walikuwa chimbuko la utawala wa mabavu na ukatili uliodumu kwa miaka 25 kuanzia 1977 hadi 2012 wa ambapo Mengistu Haile Mariam.

Mengistu aliyeongoza kupinduliwa Mfalme Haile Selassie, alitawala hadi 1991 alipokimbilia Zimbabwe, na uongozi uliomfuatia ulikuwa wa Meles Zenawi, aliyefariki Agosti 2012 .

Abiy Ahmed alipochaguliwa mapema mwaka 2018, alianza mageuzi na kutafuta amani na majirani hasa Eritrea ila matatizo ya awali na hasa ugomvi wa kina wa vyama shindani vya ukombozi vilivyojikita katika majimbo, uliendelea.

Ethiopia imeendelea kuwa katika kibano kutoka Marekani na mataifa mengine ya Magharibi baada ya kutoa amri kwa maofisa saba wa ngazi za juu wa mashirika ya Umoja wa Mataifa wanaofanyakazi nchi humo kutimuliwa.

Wanafukuzwa na Abiy anayesema wanajiingiza katika mambo ya ndani ya nchi hiyo, lakini tatizo ni kushindwa kupeleka misaada jimbo la Tigray ambayo kwa sehemu kubwa imeshikiliwa na wababe wa vita wa jimbo hilo wanaopigania kujitenga na utawala wa Addis Ababa, baada ya kuondolewa madarakani kwa ujio wa Abiy.

Walifanya uchaguzi mapema wakati uchaguzi ukiahirishwa, wakapuuzia suala la corona, na kuanza kutawala jimbo hilo watakavyo wao.

Wachambuzi wa habari wanasema kuwa Ethiopia ilisukumwa na Marekani kuacha siasa za kibabe za kimapinduzi baada ya shambulio la Septemba 11, 2001 nchini Marekani, lililobomoa majengo ya kituo kikuu cha biashara na kuivamia Wizara ya Mambo ya Nje, ingawa hatua hiyo haikubadili mwelekeo.

Kwa Ethiopia kama ilivyokuwa nchini Myanmar, wapokeaji wa Nishani ya Nobel sasa ndiye wakandamizaji. Abiy anaonekana kama 'dikteta' anayezuia misaada ya kibinadamu kuingia Tigray, akiamini inakwenda kuwanufaisha waasi wanaompinga kama ilivyo Burma mama aliyepokea nishani hiyo alirudi jela akituhumiwa kuwa sehemu ya mauaji ya kimbari ya Warohingya.

Hali hiyo ni kielelezo cha usemi wa Rais Samia Suluhu Hassan akimnukuu Mwalimu Nyerere zamani kuwa 'demokrasia siyo Coca-Cola' ambayo inafanana kokote uendako duniani. Jambo la msingi ni kuwa demokrasia inachukulia kuwa takriban watu wote wanapenda amani ila wapo watawala wenye kutotaka kuwajibika, wakati yapo makundi ya watu ambayo bila 'mkono wa chuma' wataiharibu nchi.

Kiongozi wa Myanmar Aung San Suu Kyi , alifika kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Haki za Binadamu (ICJ) kulitetea taifa hilo dhidi ya mauaji ya kimbari yaliyowaangamiza maelfu ya Warohingya na wengine zaidi ya 700,000 kukimbilia Bangladesh, mwaka 2017.



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Mengistu aliyeongoza kupinduliwa Mfalme Haile Selassie, alitawala hadi 1991 alipokimbilia Zimbabwe, na uongozi uliomfuatia ulikuwa wa Meles Zenawi, aliyefariki Agosti 2012 .



Kiongozi wa zamani wa Burma, Suu Kyi, washindi wa Tuzo ya Nobel wanaokwaza haki za binadamu.



## Wanawake watakiwa kuhamasisha sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAWAKE wametakiwa kuunga mkono jitihada za Rais Samia Hassan Suluhu za kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwakani.

Mwenyekiti wa kinamama Jimbo la Makao makuu Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Shele Sheshu, alitoa wito huo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuhamasisha kundi hilo kwenye sensa ya mwezi Agosti mwakani.

Alisema ni muhimu zoezi hilo la sensa likafanikiwa ili kuiwezesha serikali kupata idadi kamili itakayowezesha kupanga mipango ya maendeleo.

Aidha, alisema wanawake kwa asilimia kubwa ndiyo wanaoishi na familia majumbani, na wana kila sababu ya kuhakikisha wanashiriki vyema katika utoaji taarifa sahihi za watu na makazi.

"Wanawake kwa asilimia kubwa ndiyo wanaoishi na familia kwenye kaya, kwa maana hiyo wana nafasi kubwa katika kushirikiana na serikali wakati utakapofika wa zoezi hilo la sensa ya watu na makazi," alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliziomba familia zinazoishi na wazee vikongwe na wenye ulemavu kutowaficha majumbani kwa kuwa watawakosesha haki yao ya msingi ya kuhesabiwa.

Alisema haki ya kuhesabiwa ni ya kila Mtanzania bila kujali kuna wazee vikongwe na wenye ulemavu, wote wanastahili kupatiwa maendeleo.

Alisema bado kuna ukatili na unyanyapaa baadhi ya familia zinazoishi wa wazee vikongwe na wenye ulemavu wa kuwaficha majumbani na kusababisha kuwakosesha haki yao ya msingi ya kuhesabiwa kwenye sensa.

Hata hivyo, Mwenyekiti huyo aliwaomba Watanzania kutolihusisha sensa ya watu na makazi na imani ya dini.

Alisema sensa halifungamani na imani yoyote ya dini kwa kuwa lipo kwa ajili ya serikali kupanga mipango yake ya maendeleo.

"Viongozi wa dini kwa kushirikiana na serikali wanatakiwa kutoa elimu itakayohakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu ili kupata idadi kamili ya watu wake," alisisitiza.

# Wanaotaka mabadiliko ya Katiba wapewa angalizo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amewataka wananchi wanaohitaji mabadiliko ya Katiba wahakikishe wanafahamu kero zilizopo kwenye utekelezaji wa vifungu vya sheria vilivyopo kabla ya kupendekeza vifungu vipya.

Jaji Mkuu alitoa wito huo jijini hapa alipokuwa akimuapisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Elieza Feleshi kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Prof. Juma alisisitiza kuwa ni vyema vifungu vya sheria vinavyotumika vikatekelezwa kwa ufanisi ili kuleta matokeo zaidi kabla ya kufikiri kufanya mabadiliko.

"Kwa hiyo wananchi tunapotaka mabadiliko ya sheria, katiba tuhakikishe vifungu vilivyopo sasa tumevipa utekelezaji, tujue kuna changamoto gani katika utekelezaji wa vifungu vilivyopo kabla ya kufikiria kwamba pengine kuna vifungu vingine huko nje ndiyo vinaweza kuleta matokeo bora zaidi," alisema.

"Kwa hiyo sheria zetu sio mbaya, nafsi ndiyo mbaya, sheria hii hii ukiipeleka Marekani itafanya kazi vizuri sana, kwa hiyo badala ya kufikiria mabadiliko ya sheria sana, tuanze kufikiria mabadiliko ya nafsi, nafsi zetu ziheshimu sheria zifuate utaratibu kwa sababu bila sisi wenyewe kufuata utaratibu hata tuwe na sheria nzuri namna gani haitatusadia."

Jaji Mkuu huyo alisema wananchi wanapokuwa na malalamiko watumie mifumo iliyopo kutoa malalamiko yao ili mamlaka zinazohusika zipime kama inatosha ili kama haitoshi ndipo ifanyiwe mabadiliko.

"Kwa hiyo mimi ningeomba wananchi watumie mifumo iliyopo kulalamika kuhusu masuala ya kinidhamu dhidi ya kiongozi yeyote yule ndani ya mahakama ili malalamiko yao yashughulikiwe maana hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria," alisisitiza.

Vile vile, Jaji Mkuu alitoa wito kwa wananchi wenye malalamiko ya kinidhamu dhidi ya majaji na mahakimu kufuata taratibu za kuwasilisha malalamiko hayo katika kamati ya nidhamu ya majaji ili kuchukuliwa hatua.

Awali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Feleshi aliahidi kuwa ataitumikia nafasi hiyo kwa weledi mkubwa kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla.




Shehe wa Wilaya ya Bahi, Sulaimani Twalibu (kushoto), akishirikiana na Shehe wa Kata ya Chibelela, Sudi Sakela (kulia), kuzindua jiwe la msingi la ujenzi wa msikiti unaojengwa katika kijiji cha Chibelela, Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yafanyia marekebisho uongozi NARCO

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imefanyia marekebisho uongozi wa kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika sekta ya mifugo na nyama nchini.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Mkurugenzi Mkuu wa NARCO, Prof. Peter Msoffe, alisema mfumo huo mpya wa uongozi unatarajia kuanza kabla ya mwisho wa mwaka huu ambao utahusisha kurugenzi kuu mbili.

"Kurugenzi ya kwanza itakuwa inajishughulisha na masuala ya uzalishaji, uendelezaji wa miundombinu na opereshani," alisema.

Alisema kurugenzi hiyo itakuwa na sekta kuu tatu ambazo zitajikita katika kushughulikia masuala ya upimaji na uendelezaji wa miundombinu, operesheni udhibiti wa magonjwa pamoja na malisho ya mifugo.

"Kurugenzi ya pili itakuwa na jukumu la kuangalia na kusimamia masuala ya huduma kwa walaji (watumiaji wa bidhaa za NARCO) na itakuwa na sekta kuu mbili," alisisitiza.

Alisema sekta ya kwanza itajikita katika upande wa rasilimali watu na uongozi na sekta ya pili itajihusisha na mipango, usimamiaji wa shughuli na upembuzi.

Aidha, alisema mfumo huo mpya wa uongozi pia utahushisha uimarishaji na uendelezaji wa vitengo muhimu kama vile, kitengo cha manunuzi, teknolojia ya habari na takwimu, usimamiaji wa fedha, masoko pamoja na mahusiano ya umma.

"Kwanza kabisa, tunaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa ajili ya jitihada zake za kuboresha ufanisi wa kampuni ya Ranchi ya Taifa, na ni matumaini yetu kwamba mfumo huu mpya wa uongozi utaleta chachu kubwa ya maendeleo, siyo kwa NARCO peke yake, bali kwa sekta nzima ya mifugo na nyama Tanzania," Msofe alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa Narco inaendelea na jitihada za kukagua na kuweka mipaka katika vitalu vyake vyote nchini ili kukabiliana na wimbi la uvamizi wa maeneo hayo muhimu.

Kwa sasa, NARCO ina jumla ya vitalu 14 vilivyo katika maeneo tofauti nchini na ambavyo vipo chini ya usimamizi wa jumla ya wawekezaji wakubwa 120, na wawekezaji wadogo 200.



# RC atengua uamuzi wa madiwani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametengua uamuzi wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ambalo lilipitisha sheria ndogo la kumtoza Sh. 1,000 kila mtu anayetembelea ufukwe wa Matema katika Ziwa Nyasa.

Lengo la kupitisha sheria ya kutoza fedha hizo ni kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri inayopakana na nchi jirani ya Malawi.

Homera alifikia uamuzi huo juzi wakati akiongoza kongamano la siku moja la kujadili fursa za kiuchumi na uwekezaji lilifanyika jijini Mbeya na kuratibiwa na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Mbeya.

Katika uamuzi huo, Homera alisema hawezi kukubali kuona wananchi wakitozwa fedha ya kiingilio wakati wanakwenda kupunga upepo kwenye ufukwe wa Matema na kueleza kuwa kitendo hicho ni cha kushangaza na cha kwanza kutokea nchini.

Mkuu huyo wa Mkoa aliiagiza serikali ya Wilaya ya Kyela kushughulikia hilo jambo haraka kwa kuwa linaleta picha mbaya kwa watalii wanaotaka kwenda kutembelea fukwe hizo.

"Huu ni ufukwe wa kwanza nchini kuwatoza watu fedha za kiingilio. Mimi nitakuwa mtu wa mwisho kuunga mkono hili jambo. Huo si utaratibu hata kama ni sheria ndogo ndogo, mamlaka niliyo nayo yanasema mkuu wa mkoa ana uwezo wa kutengua uamuzi wa baraza la madiwani ambao hauna tija kwa wananchi," alisema.

Kuhusu fursa za kiuchumi, Homera alisema mkoa wa Mbeya una fursa nyingi, hivyo kuwaomba wafanyabiashara na wawekezaji kujitokeza kuchangamkia fursa hizo kwa kuwekeza katika maeneo mbalimbali.

Aliitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mbeya kujenga mazingira rafiki ya kukusanya kodi na kwamba hawapaswi kutumia nguvu au kuchukua fedha za wafanyabiashara kinyume CHA sheria za ukusanyaji wa kodi.

"Watu wa mapato ikiwezekana muwe mnawapa hata soda wateja wenu wakija. Hata pale mapokezi mnawaweka wadada wenye sura nzuri na wenye lugha ya ukarimu ili mteja avutiwe kupeleka kodi mwenyewe. Sitapenda kusikia malalamiko ya wafanyabiashara kwamba wananyanyaswa, "alisema.

Nae Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mbeya, Erick Sichinga, alisema mazingira bora ya uwekezaji yatawavutia wafanyabiashara kuwekeza kupitia sekta mbalimbali mkoani Mbeya ikiwamo uanzishwaji wa viwanda.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akimpatia viroba vya maziwa mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mwenge ya jijini Mbeya, Josephine Lawrence, wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya unywaji maziwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'Tumieni redio kuhamasisha utalii'

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WADAU wa Utalii nchini wameshauriwa kutumia vyombo vya habari zikiwamo redio za kijamii kuhamasisha utalii wa misitu, ili kuongeza maduhuli ya serikali yanayotokana na viingilio kwenye hifadhi za misitu.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Highlands FM ya jijini Mbeya, Jacqueline Mwakyambiki, wakati wafanyakazi wa kituo hicho na wadau wao walipotembelea Mlima Rungwe kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani.

Mwakyambiki alisema vyombo vya habari husasani redio za kijamii, zinazopatikana mikoani zina nafasi kubwa kuhamasisha utalii wa ndani ukiwamo wa misitu kwa kuwa vyombo hivyo vinasikilizwa na watu wengi katika maeneo husika.

Alisema kwa kutambua hilo, kituo chake kiliamua kuratibu matembezi ya kupanda Mlima Rungwe ambayo yaliwashirikisha zaidi ya wadau 70 kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya.

"Redio za kijamii zikitumika ipasavyo kuhamasisha utalii wa ndani, wananchi wengi watahamasika ukizingatia kuwa mkoa wetu una vivutio vingi sana lakini mwamko wa wenyeji kutembelea ni mdogo kwa kuwa hakuna hamasa. Suluhu inaweza kuwa kutumia hizi redio zetu," alisema.

Ofisa Utalii wa Hifadhi Asilia ya Misitu wa Mlima Rungwe, Jesca Mgata, alisema hifadhi hiyo ni eneo mojawapo lenye vivutio vya utalii vinavyotumika kwa ajili ya utalii ikolojia, utafiti, burudani za kutembea na mapumziko.

Alisema utalii wa Mlima Rungwe unasimamiwa na kuendeshwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Alisema wakiwa wadau wa utalii, wanaamini uhifadhi wa misitu ni muhimu katika kuchochea maendeleo ya utalii.

"Katika mlima huu kuna viumbe mbalimbali wanapatikana hapa wakiwamo kapunji ambao hawapatikani sehemu yoyote Afrika. Pia kuna mimea aina mbalimbali, hivyo ni sehemu ambayo ukiitembelea utaifurahia kutokana na kuwapo kwa vivutio vingi," alisema.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya kupandia mlima huo, Lameck Charles, alisema matembezi hayo yamewashirikisha wadau mbalimbali kama vile benki, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wafanyabiashara na wasikilizaji.

# Mil. 500 kujenga Chimala – Kapunga

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

KATIKA kuhakikisha wananchi wananufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo, serikali wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chimala-Kapunga yenye urefu wa kilomita 26.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema eneo la Kapunga ni miongoni mwa maeneo wilayani hapa yenye wawekezaji wakubwa yakiwapo mashamba makubwa ya Kapunga Estate na wakulima wadogo, hivyo barabara hiyo ni muhimu.

"Kwa muda mrefu wananchi walikuwa wanaahidiwa kwamba barabara hii itaboreshwa, sasa tumeshapokea fedha hizi na tumeshatoa maelekezo kwa maofisa wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili waanze kuijenga," alisema Mfune.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwemo kulinda vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi wa mradi huo ili visiibwe na kukubali kupisha mradi huo kwa wale ambao watalazimika kuhamishwa.

Pia alisema halmashauri ya wilaya hiyo imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya inayojengwa katika eneo la Rujewa ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Mfune pia alisema wanaendelea kushirikiana na wananchi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa 127 ili kukabiliana na uhaba wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotarajia kuanza masomo Januari, mwakani.





# Waziri aelekeza tathmini ya vifaa taasisi ya UDSM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Da es Salaam kilichopo Zanzibar kimetakiwa kufanya tathmini kujua gharama halisi za vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kufundishia.

Hatua ya kutaka kufanyika kwa tathmini hiyo inafuatia baada ya kuteketea kwa jengo hilo kwa moto wiki iliopita.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alipofanya ziara na kukagua jengo la taasisi ya hiyo lilopo Malinndi Zanzibar lililoathirika na moto na kusababisha hasara kubwa.

Alisema kufanyika kwa tathmini ya haraka kwa kiasi kikubwa kutaisaidia na kuiwezesha serikali kurudisha huduma za kufundishia wanafunzi kwa kuwapatia vifaa vipya .

Alisema kwamba taasisi ya Sayansi ya Baharini ya UDSM ni muhimu zaidi kutokana na vipaumbele vya serikali zote mbili Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuimarisha uchumi wa bluu na masuala ya utafiti wa baharini na rasilimali zake.

Prof. Nalichako, alisema kuelekea katika uchumi na kufaidika kwa matumizi ya rasilimali za baharini masuala ya utafiti yanahitajika kwa kiasi kikubwa ili wananchi wafaidike na sekta mbalimbali ukiwamo uvuvi wa bahari kuu.

"Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu ni miongoni mwa vitengo vinavyotegemewa na serikali katika masuala mbalimbali ikiwamo ya utafiti wa baharini na rasilimali zake kuwanufaisha wananchi ikiwamo na mazao ya baharini." alisema.

Naye Makamu mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema moto huo umesababisha hasara ya vifaa mbalimbali ambavyo vilikuwa vinatumiwa na wanafunzi kwa ajili ya masomo ya vitendo.

Alisema tathmini ya kina na haraka itafanywa na uongozi wa Taasisi hiyo ili kupata fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya kununua vifaa vya mafunzo ya vitendo.

Mkuu wa Kikosi cha Zimamoto Zanzibar, Rashid Mzee, alisema moto huo ulizuka juzi alasiri ambapo hata hivyo, chanzo chake hakijafahamika na uchunguzi unaendelea.

"Tulipata taarifa ya moto saa 9.40 na tulifika na kuanza kuzima moto, ingawa chanzo chake hakijafahamika hadi sasa," alisema.

# Mwalimu madrasa matatani madai kulawiti wanafunzi 5

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linamshikilia mwalimu wa madrasa, Ali Abdallah Ali (32), kwa tuhuma za kulawiti wanafunzi wake watano.

Mtuhumiwa huyo mkaazi wa Mweza Mkoa wa Mjini Mgharib Unguja anadaiwa kuwawiti watoto hao wa kiume wenye umri kati ya miaka 11 na wengine miaka sita.

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Omar Said Nassir, alisema mtuhumiwa huyo pia ni mwalimu katika Shule binafsi ya Taifa iliyokuwepo eneo la Regezamwends Wilaya ya Magharibi 'A' Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Aidha, alisema mtuhumiwa aligundulika baada ya kumlawiti mtoto mmoja kati ya wanne waliogundulika baadae ambao ni wanafunzi wake katika madrasa.

Alisema tukio hilo la udhalilishaji liliripotiwa kituo cha Polisi Mwera Oktoba 2, mwaka huu majira ya asubuhi ambapo wazazi wa watoto hao walipatwa na wasiwasi na kuwapeleka watoto wao kituo cha polisi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.

Kamanda huyo alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akiwalawiti watoto hao nyumbani kwake.

Kamanda Nassir alisema kwamba mtuhumiwa huyo yupo chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi, huku wakiendelea na upelelezi na kwamba utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

Aliwaomba wazazi na walezi kufuatilia mienendo ya watoto wao mara kwa mara na kuwa nao karibu ili kubaini matatizo yanayowakabili.

"Tukae na watoto wetu mara kwa mara na kuwachunguza na kuwakagua, kwani itatusaidia kujua vitendo vya udhalilishaji dhidi yao mapema na kuchukua hatua," alisema.

Kamanda Omary, aliwasisitiza wananchi hasa vijana wa kiume kuacha kutenda makosa ya udhalilishaji kwa tamaa zao.

Alisema pia mshitakiwa Samson Rafael Juakali (21), mkaazi wa Fuoni Kipungani, amehukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kosa la kumtorosha, kumbaka na kumpa ujauzito mtoto mwenye miaka 15 (jina limehifadhiwa).




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Balozi wa Nigeria hapa nchini, Hamisu Umar Takamawa, alipofika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# SMZ yataka uwekezaji hospitali za kisasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inakaribisha wawekezaji kuwekeza katika miradi ya ujenzi wa hospitali za kisasa.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, na kueleza kwamba hospitali hizo ni zitakazosaidia kutoa matibabu kwa magonjwa ambayo hupatikana nje ya nchi.

Mazrui alikuwa akizungumza na mfanyabiashara kutoka Dubai, Ahmad Al-Falasi, ambaye anatarajia kujenga hospitali kubwa ya kutibu magonjwa yasiyoambukiza.

Waziri Mazrui alisema Zanzibar inahitaji hospitali ya kisasa yenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali ikiwamo yasiyoambukiza ambayo yanaongoza kwa kusababisha vifo.

Alisema wanamkaribisha mfanyabiashara huyo kujenga hospitali ya aina hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza mzigo wa serikali kuwasafirisha wagonjwa kwenda njeya nchi.

"Zanzibar inahitaji huduma za afya bora, ambazo zitasaidia kukabiliana na changamoto ya mgonjwa tishio yanayosababisha vifo kwa wananchi wengi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi (ZIPA), Sharifu Ali Sharifu, amesema wapo katika hatua ya mwisho ya kuchagua eneo ambalo litajengwa hospitali hiyo huko Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema eneo la Fumba lipo katika ukanda wa maeneo huru ya uchumi na uwekezaji, ambayo yametengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ikiwamo ya uchumi na maendeleo.

Mwekezaji, Ahmada Al-Falasi, alisema nia yake ni kujenga hospitali kubwa yenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali hatua ambayo itapunguza kusafirisha wagonjwa kwenda nje ya nchi.

"Nimetembelea maeneo mengi kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa, lakini nimechagua Zanzibar kutimiza ndoto yangu ya kuwa na hospitali kubwa ya kisasa ya kutoa tiba," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

KIWANJA KINAUZWA KIPO KISUKURU JKT SEGEREA DAR ES SALAAM, UKUBWA SQM 2252, KINA HATI, BEI 60 MILIONI. **MAWASILIANO: 0655 857523.**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999 (SURA 113)**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI**

**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: MWALIMU CHATA MOHAMED**

**ARDHI: KIWANJA NA. 13 KITALU 'B' ENEO LA TEMEKE MANISPAA YA TEMEKE DAR ES SALAAM**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI,** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti.

**BARUA HALISI YA TOLEO** ikipatikana irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MINISPAA YA TEMEKE S.L.P 46343, DAR ES SALAAM.**

P.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

216493502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 374.2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU GABRIEL M. MAKANILE WA KIGOGO FRESH**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA AGATHA KASWENDA MAKANILE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnano tarehe 04 Mwezi wa 11 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hayateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 01 Mwezi wa 10 Mwaka 2021.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA ILALA

216493602

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

116491502

**Grite Friday Mwakasungula**

Anatangaza kupotelewa na Ofa ya Kiwanja namba 175 Kitalu "EE" kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Grite Friday Mwakasungula kwa simu namba **0753236526.**

**Rbnamba SHY/RB/ 2021/ Control namba 9910830452712.**

Naomba kuwasilisha.

Josephat P. Mushi
AFISA ARDHI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

216493902

## KUPOTEA KWA CHETI



216494002

**SELEMANI KEPHA YORAM** anatangaza kupotelewa na CHETI CHA KIDATO CHA NNE yenye No **S.0123.0091** kilichotolewa na KWIRO SECONDARY SCHOOL mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/424311/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO.**

**Kituo cha CHAMWINO IKULU Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 08 /2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JUMA SEIF MWINYIKAMBI WA CHAMWINO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NEEMA SEIF JUMA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 10 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 10 mwaka 2021.

216494102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo PONGWE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 38/2021**

**Ombi la SAID ALLY MSANGA Kuteuliwa**

**Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ALLY SAID MSANGA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 19/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 28/09/2021.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

216494202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EBEARTH KAHIGI KASENENE** amepoteza kadi ya gari namba **T 438 CNC** na taarifa imetolewa katika kituo cha Polisi Kayanga Wilayani Karagwe kwa kumbukumbu namba **KAG/KAY/RB/337834/2021.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

216494302

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TEDDY SITIMI SILIWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAUJAE** yenye namba za usajili **MC 676 ADR. Chasis No. * LC6PCJK26J0055494.** Engine No. 156FM1-5A. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/467418/2021.**

216494402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo ……….............**
**MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi…………….135…………2021**
**Ombi la………IBRAHIMU HAMISI HUSSEIN Kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**……………………………………………………….**
**HAMISI HUSSEIN MANDE**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 23/9/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 2/9/2021**

116494502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SAMWEL SAMSON NSWILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.348 CRM** AINA YA **TOYOTA ALTEZZA.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILCHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/480103/2021**

216494602

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ELIKADO MHOZA BARNABA anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 172 CCZ.Chasis No. MD2A21BYTJWH88117, Engine No. PFZWJH77481. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/477993/2021.

116495302

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA GARI.

VENANTIUS PHILMATUS GABERUS anatangaza kupotelewa na kadi za **PIKIPIKI** aina ya **BOXER,** yenye namba za usajili **MC 316 CSZ, SANLG** yenye namba ya usajili **MC 501 BQF,** Na kadi ya Gari aina **TOWN HIACE** yenye namba za usajili **T 359 DUL.**Yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi DOM/DOM/RB/478874/2021.

116495402

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI.

VENANTIUS PHILMATUS GABERUS anatangaza kupotelewa na kadi za **PIKIPIKI** aina ya **BOXER,** yenye namba za usajili **MC 192 CJM, MC 838 CJS na MC 247 CJX** Yenye majina ya **MOHAMMED-ENTERPRIS-ES(T)LTD.**Yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOM/DOM/RB/478874/2021.**

116495402

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA ZA GARI.

VENANTIUS PHILMATUS GABERUS anatangaza kupotelewa na kadi za **PIKIPIKI** aina ya **KINGLION,** yenye namba za usajili **MC 156 CLU** Yenye jina la **TEDDY MICHAEL KUSUNDWA, SANLG** yenye namba ya usajili **MC 814 CQM** Yenye jina la **SANLG LIMITED** Na kadi za Gari aina **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 296 DSC** Yenye jina la **HENRY NOHA MAGAWA, T 588 BQD** Yenye jina la **FORTUNATUS KANTY TILLO.**Yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi DOM/DOM/RB/478874/2021.

116495402

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ATHUMANI DAUDI LEMA, Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki Yenye namba za usajili MC 754BWR Engine namba 162FMJSS7G04414 namba Chassis namba LFSGE2PK004414 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : KIL/MOS/RB/468845/2021

116495502

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza

Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Katika kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, Serikali imerekebisha tozo mbalimbali kwa taasisi zote zinazotoza tozo kwenye biashara ya mafuta hapa nchini.

Uamuzi huo ulifikiwa leo, **tarehe 5 Oktoba 2021**, baada ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuitisha kikao cha kujadiliana namna bora ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini na kuhakikisha kunakuwepo na utangamano wa hifadhi ya mafuta (security of supply), lakini pia kuwahakikishia wafanyabiashara wa mafuta hapa nchini wanafanya biashara katika na mazingira mazuri.

Baada ya maagizo hayo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatoa taarifa kwa umma juu ya tozo ambazo Serikali imepunguza kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko kubwa la bei za mafuta hapa nchini kama ilivyoainishwa hapa chini:-

a) Serikali imebadilisha tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari (wharfage) ambayo inatozwa kwa dola za Marekani (USD 10/MT + VAT) kwa tani, na sasa itatozwa kwa shilingi ya Tanzania; na pia tozo hiyo imepunguzwa kufikia shilingi 15 kwa lita kutoka wastani wa shilingi 22 kwa lita na kuondoa VAT katika tozo hii. Hii ni kwa sababu sehemu ya tozo hii iliwekwa kwa ajili ya ujenzi wa boya la kupokelea mafuta baharini (Single Bouy Mooring - SBM) ambao kwa sasa umekamilika na hivyo kiasi cha shilingi 15 kwa lita kinachopendekezwa kinaweza kutumika kwa ajili ya matengenezo (maintenance). Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 23.15 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

b) Serikali imepunguza tozo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kuchakata nyaraka (Customs processing fees) kutoka shilingi 4.8 kwa lita na kuwa kiwango maalumu cha shilingi milioni ishirini (20) kwa kila meli ambapo kwa wastani, meli 7 huleta shehena ya mafuta kila mwezi. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 14.79 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

c) Serikalli imepunguza tozo ya Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) kwa shilingi moja kwa lita na kuwa tozo ya kiwango maalumu ambacho ni shilingi milioni 7 kwa kila meli badala ya kutozwa kwa kila lita. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 2.85 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

d) Serikali pia imepunguza tozo ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ya kupima ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini kutoka shilingi 1.24 kwa lita na kutozwa kwa kiwango maalumu ambacho ni shilingi milioni 12.8 kwa kila meli. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 3.21 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

e) Serikali imebadilisha mfumo wa utozaji wa tozo kwa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kutoka shilingi 3.54 kwa lita na kuwa tozo ya kiwango maalumu ambacho ni shilingi milioni 20 kwa kila meli. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 10.45 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

f) Tozo kwa ajili ya shughuli za udhibiti za EWURA nazo zimepunguzwa kutoka wastani wa shilingi 5.54 kwa lita hadi shilingi 3.06 kwa lita. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 3.45 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

g) Serikali pia imefuta tozo ya huduma (Service Levy) inayotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Halmashauri za Temeke na Kigamboni (Dar es Salaam), Tanga na Mtwara kwa wafanyabiasha wa jumla ambao wana maghala ya kuhifadhia mafuta ya jumla. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 19.82 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

h) Pia, Serikali imepunguza gharama za kuweka vinasaba kwenye mafuta kutoka shilingi 14 kwa lita hadi shilingi 7 kwa lita. Mabadiliko haya yataleta nafuu kwa watumiaji mafuta kwa wastani wa shilingi bilioni 23.92 kwa mwaka kutokana na matumizi ya lita bilioni 3.42 kwa takwimu za mwaka 2020.

Kiujumla marekebisho haya yatawanufaisha Watanzania kwa kupunguza matumizi ya fedha kwenye manunuzi ya mafuta kwa shilingi bilioni 102 kwa mwaka. Mfano, bei za petroli kwa Dar es Salaam kuanzia tarehe 6 Oktoba 2021 zilitakiwa ziongezeke kwa shilingi 145 kwa lita lakini kwa hatua zilizochukuliwa na Serikali, bei hizo zimeongezeka kwa shilingi 12 kwa lita.

Kutokana na hatua hizi bei za mafuta kuanzia kesho Jumatano ya Tarehe 6 Oktoba 2021 zinakuwa kama ifuatavyo:-

## BEI ZA REJA REJA ZA MAFUTA KUANZIA TAREHE 6 OKTOBA 2021

| MJI | BEI KIKOMO | | |
|---|---|---|---|
| | Petroll (TZS/Lita) | Dizeli (TZS/Lita) | Mafuta ya Taa (TZS/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **2,439** | **2,261** | **2,188** |
| **Arusha** | **2,535** | **2,301** | **2,272** |
| Arumeru (Usa River) | 2,535 | 2,301 | 2,272 |
| Karatu | 2,553 | 2,320 | 2,290 |
| Longido | 2,546 | 2,312 | 2,283 |
| Monduli | 2,540 | 2,307 | 2,277 |
| Monduli-Makuyuni | 2,545 | 2,311 | 2,282 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,619 | 2,386 | 2,363 |
| **Pwani (Kibaha)** | **2,443** | **2,266** | **2,192** |
| Bagamoyo | 2,450 | 2,272 | 2,199 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,480 | 2,303 | 2,229 |
| Chalinze Junction | 2,453 | 2,275 | 2,202 |
| Chalinze Township (Msata) | 2,457 | 2,279 | 2,206 |
| Kibiti | 2,459 | 2,281 | 2,208 |
| Kisarawe | 2,446 | 2,268 | 2,195 |
| Mkuranga | 2,448 | 2,271 | 2,197 |
| Rufiji | 2,466 | 2,289 | 2,215 |
| **Dodoma** | **2,497** | **2,320** | **2,246** |
| Bahi | 2,505 | 2,327 | 2,254 |
| Chamwino | 2,493 | 2,315 | 2,242 |
| Chemba | 2,524 | 2,346 | 2,273 |
| Kondoa | 2,530 | 2,353 | 2,279 |
| Kongwa | 2,495 | 2,317 | 2,244 |
| Mpwapwa | 2,498 | 2,321 | 2,247 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 2,510 | 2,333 | 2,259 |
| Mtera (Makatopora) | 2,516 | 2,339 | 2,265 |
| Mvumi | 2,504 | 2,326 | 2,253 |
| **Geita** | **2,604** | **2,427** | **2,353** |
| Bukombe | 2,593 | 2,415 | 2,342 |
| Chato | 2,625 | 2,448 | 2,374 |
| Mbogwe | 2,642 | 2,465 | 2,391 |
| Nyang'hwale | 2,619 | 2,442 | 2,368 |
| Iringa | 2,503 | 2,325 | 2,252 |
| Ismani | 2,508 | 2,330 | 2,257 |
| Kilolo | 2,507 | 2,330 | 2,256 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,513 | 2,335 | 2,262 |
| Mufindi (Igowole) | 2,521 | 2,344 | 2,270 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,654** | **2,477** | **2,403** |
| Biharamulo | 2,628 | 2,451 | 2,377 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,670 | 2,493 | 2,420 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,676 | 2,499 | 2,425 |
| Muleba | 2,654 | 2,477 | 2,403 |
| Ngara | 2,642 | 2,464 | 2,391 |
| Misenyi | 2,663 | 2,485 | 2,412 |
| **Katavi (Mpanda)** | **2,647** | **2,469** | **2,396** |
| Mlele (Inyonga) | 2,666 | 2,488 | 2,415 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,639 | 2,462 | 2,389 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,664 | 2,487 | 2,413 |
| **Kigoma** | **2,670** | **2,493** | **2,419** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,682 | 2,505 | 2,431 |
| Buhigwe | 2,659 | 2,482 | 2,408 |
| Kakonko | 2,627 | 2,450 | 2,376 |
| Kasulu | 2,656 | 2,479 | 2,405 |
| Kibondo | 2,634 | 2,457 | 2,383 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,524** | **2,291** | **2,261** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,528 | 2,294 | 2,265 |
| Mwanga | 2,517 | 2,284 | 2,254 |
| Rombo (Mkuu) | 2,541 | 2,308 | 2,282 |
| Same | 2,511 | 2,277 | 2,248 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,531 | 2,298 | 2,268 |
| **Lindi** | **2,468** | **2,293** | **2,246** |
| Lindi-Mtama | 2,473 | 2,297 | 2,265 |
| Kilwa Masoko | 2,492 | 2,317 | 2,221 |
| Liwale | 2,504 | 2,328 | 2,267 |
| Nachingwea | 2,488 | 2,313 | 2,276 |
| Ruangwa | 2,494 | 2,319 | 2,277 |
| **Manyara (Babati)** | **2,569** | **2,335** | **2,310** |
| Hanang (Katesh) | 2,579 | 2,346 | 2,321 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,584 | 2,351 | 2,321 |
| Mbulu | 2,582 | 2,348 | 2,323 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,601 | 2,368 | 2,342 |
| **Mara (Musoma)** | **2,617** | **2,440** | **2,366** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,658 | 2,480 | 2,407 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,626 | 2,449 | 2,375 |
| Rorya (Shirati) | 2,661 | 2,483 | 2,410 |
| Bunda | 2,608 | 2,431 | 2,357 |
| Bunda (Kisorya) | 2,618 | 2,440 | 2,367 |
| Butiama | 2,614 | 2,437 | 2,363 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,663 | 2,485 | 2,412 |
| Tarime | 2,628 | 2,451 | 2,377 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,633 | 2,455 | 2,382 |

**Inaendelea Uk 20**

## HABARI MICHEZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mbeya** | **2,546** | **2,368** | **2,295** |
| Chunya | 2,555 | 2,378 | 2,304 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,560 | 2,383 | 2,310 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 2,562 | 2,385 | 2,311 |
| Kyela | 2,561 | 2,384 | 2,310 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,530 | 2,352 | 2,279 |
| Rujewa (Madibira) | 2,543 | 2,366 | 2,292 |
| Rujewa (Kapunga) | 2,540 | 2,362 | 2,289 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,555 | 2,377 | 2,304 |
| **Morogoro** | **2,464** | **2,286** | **2,213** |
| Mikumi | 2,479 | 2,302 | 2,228 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,501 | 2,324 | 2,250 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,524 | 2,346 | 2,273 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,513 | 2,335 | 2,262 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,512 | 2,335 | 2,261 |
| Malinyi | 2,522 | 2,345 | 2,271 |
| Kilosa | 2,482 | 2,304 | 2,231 |
| Gairo | 2,482 | 2,304 | 2,231 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,474 | 2,297 | 2,223 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,464 | 2,286 | 2,213 |
| Turian | 2,489 | 2,311 | 2,238 |
| **Mtwara** | **2,455** | **2,279** | **2,260** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,491 | 2,316 | 2,309 |
| Masasi | 2,471 | 2,295 | 2,286 |
| Newala | 2,476 | 2,300 | 2,292 |
| Tandahimba | 2,469 | 2,293 | 2,285 |
| Nanyamba | 2,469 | 2,293 | 2,285 |
| **Mwanza** | **2,589** | **2,411** | **2,338** |
| Kwimba | 2,607 | 2,429 | 2,356 |
| Magu | 2,597 | 2,419 | 2,346 |
| Misungwi | 2,583 | 2,406 | 2,332 |
| Sengerema | 2,621 | 2,444 | 2,370 |
| Ukerewe | 2,648 | 2,471 | 2,397 |
| **Njombe** | **2,531** | **2,354** | **2,280** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,552 | 2,374 | 2,301 |
| Ludewa | 2,569 | 2,391 | 2,318 |
| Makambako | 2,523 | 2,346 | 2,272 |
| Makete | 2,562 | 2,384 | 2,311 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,529 | 2,351 | 2,278 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,612** | **2,434** | **2,361** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,612 | 2,434 | 2,361 |
| Kalambo (Matai) | 2,619 | 2,441 | 2,368 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,625 | 2,448 | 2,374 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,540** | **2,365** | **2,311** |
| Mbinga | 2,553 | 2,377 | 2,345 |
| Namtumbo | 2,531 | 2,356 | 2,340 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,578 | 2,403 | 2,355 |
| Tunduru | 2,505 | 2,330 | 2,370 |
| **Shinyanga** | **2,568** | **2,390** | **2,317** |
| Kahama | 2,581 | 2,404 | 2,330 |
| Kishapu | 2,596 | 2,418 | 2,345 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,599 | 2,421 | 2,348 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 2,589 | 2,412 | 2,338 |
| Salawe | 2,582 | 2,405 | 2,331 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,609** | **2,432** | **2,358** |
| Busega (Nyashimo) | 2,602 | 2,424 | 2,351 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,612 | 2,435 | 2,361 |
| Maswa | 2,600 | 2,423 | 2,349 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,607 | 2,430 | 2,356 |
| **Singida** | **2,529** | **2,352** | **2,278** |
| Iramba | 2,541 | 2,364 | 2,290 |
| Manyoni | 2,514 | 2,336 | 2,263 |
| Itigi (Mitundu) | 2,529 | 2,352 | 2,278 |
| Ikungi | 2,525 | 2,347 | 2,274 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,554 | 2,376 | 2,303 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,555** | **2,377** | **2,304** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,562 | 2,384 | 2,311 |
| Ileje | 2,559 | 2,381 | 2,308 |
| Momba (Chitete) | 2,564 | 2,387 | 2,313 |
| Tunduma | 2,559 | 2,382 | 2,308 |
| **Tabora** | **2,547** | **2,369** | **2,296** |
| Igunga | 2,547 | 2,369 | 2,296 |
| Kaliua | 2,560 | 2,382 | 2,309 |
| Ulyankulu | 2,557 | 2,380 | 2,306 |
| Nzega | 2,557 | 2,380 | 2,306 |
| Sikonge | 2,556 | 2,378 | 2,305 |
| Urambo | 2,557 | 2,379 | 2,306 |
| Uyui | 2,553 | 2,376 | 2,302 |
| Mpyagula | 2,578 | 2,401 | 2,327 |
| **Tanga** | **2,478** | **2,245** | **2,234** |
| Handeni | 2,499 | 2,265 | 2,213 |
| Kilindi | 2,514 | 2,280 | 2,248 |
| Korogwe | 2,490 | 2,257 | 2,227 |
| Lushoto | 2,500 | 2,266 | 2,236 |
| Mkinga (Maramba) | 2,485 | 2,252 | 2,248 |
| Muheza | 2,483 | 2,250 | 2,234 |
| Pangani | 2,485 | 2,251 | 2,240 |

**BEI ZA JUMLA**

| | Petroli (TZS/Lita) | Dizeli (TZS/Lita) | Mafuta ya Taa (TZS/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 2,308.90 | 2,131.57 | 2,058.93 |
| TANGA | 2,348.33 | 2,115.34 | |
| MTWARA | 2,324.95 | 2,149.78 | |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**
**TAREHE 5 OKTOBA 2021**

# TAMBWE ATAMBA KUWASHA MOTO AKIANZA NA MABAO 4

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuanza msimu kwa kucheka na nyavu mara nne wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1, dhidi ya African Lyon kwenye mechi ya fungua msimu Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, mshambuliaji wa DTB, Amissi Tambwe, amesema bado ana uwezo wa kuendelea kufanya makubwa na kuisaidia timu yake kufanya vizuri.

**Tambwe nyota wa zamani wa Klabu za Simba na Yanga, amejiunga na DTB msimu huu na tayari ameanza kwa kupa ushindi mnono.**

Akizungumza na Nipashe mshambuliaji jana, Tambwe alisema kile alichokionyesha, kwenye mchezo wa kwanza amepanga kukiendeleza katika mechi zijazo.

"Si mimi peke yangu, klabu kwa ujumla imejipanga kufanya vizuri, kwenye ligi na kuhakikisha timu inapanda daraja msimu ujao, ukiangalia kuna wachezaji wenye uzoefu mkubwa mbao wamesajiliwa, kwa pamoja tutapambana mpaka mwisho, kuona timu inachezwa Ligi Kuu msimu ujao," alisema nyota.

Alisema kwake binafsi anaona bado ana uwezo wa kupambana, kwenye Ligi Kuu na ndio sababu ya kujituma katika Ligi Daraja la Kwanza.

"Mpira wa Tanzania unafahamika, ligi zake ni ngumu na zinahitaji kupambana sana, hata hii Ligi Daraja la Kwanza ni ngumu kwa sababu kila timu imejiandaa, pia kuna timu ambazo zimetoka Ligi Kuu nazo zinapambana kutaka kurejea Ligi Kuu, tunafahamu mlima uliopo mbele yetu," aliongezea kusema Tambwe.

Aidha, alisema fedha zinazotolewa na Kampuni ya Azam Media kama bonasi kwenye Ligi Kuu nazo zinachangia kwa kiasi kikubwa Ligi Daraja la Kwanza msimu huu kuwa ngumu kutokana na kina timu kutaka kupanda daraja, ili zifaidike na pesa hizo kwa kushiriki Ligi Kuu.

## Marafiki, Ufaransa kuinua wasanii

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI na mwanzilishi wa Tamasha la Marafiki, Isack Abeneko, kwa kushirikiana na Ufaransa, wameandaa tamasha litakalofanyika jijini Dar es Salaam na Bagamoyo, likiwa na lengo la kuwajengea uwezo wasanii katika maeneo mbalimbali ya Sanaa na kuwaendeleza kimataifa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Abeneko alisema tamasha hilo litawakutanisha pamoja wasanii zaidi ya 128 wa ndani na nje, sambamba na wadau na wataalamu mbalimbali wa sanaa, kwa ajili ya kushirikishana uzoefu na maarifa kwa lengo la kuinua sanaa ya muziki nchini.

Alisema tamasha hilo litafanyika kuanzia Oktoba 7-9 kwa Dar es Salaam na Oktoba 10, mwaka huu Bagamoyo likiwa na kaulimbiu ya "Muziki na Maendeleo ya Kijamii', huku dhumuni kubwa likiwa ni kuhamasisha vijana na wanamuziki kutumia muziki kama nyenzo ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

"Tamasha la Marafiki pia litakuwa na semina za mafunzo na mjadala wa wazi kwa siku tatu, mambo mbalimbali yatajadiliwa na kutolewa elimu inayohusu namna ya kufuata utaratibu wa biashara ya muziki, utengenezaji wa muziki wenye mzunguko na unaofaa, usimamizi wa msanii na jinsi ya kupata soko la ndani na kimataifa, ili kuwaendeleza wasanii nchini," alisema Abeneko.

## *Twiga Stars yaitaka fainali COSAFA*

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kushinda mabao 3-0, dhidi ya Sudan Kusini kwenye michuano ya soka la Wanawake Ukanda wa Kusini mwa Afrika (COSAFA), Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake nchini (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema lengo lao mwaka huu ni kufika fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza juzi, baada ya mechi ya mwisho ya Kundi B, kwenye Uwanja wa Gelvandale, Port Elizabeth nchini Afrika Kusini, ambako michuano hiyo inachezwa, kocha huyo alieleza kufurahia kupata matokeo hayo, ambayo yamewawezesha kutinga hatua ya nusu fainali, lakini lengo lao mwaka huu kama wageni waalikwa ni kufika fainali.

"Nafurahi kwa matokeo haya, tumecheza vema na kupata matokeo mazuri, kipindi cha kwanza tulishindwa kupata bao, lakini cha pili tukafunga matatu, lengo letu msimu huu ni kuhakikisha tunapambana na kufika fainali, sasa tunajiandaa tuone nusu fainali tutacheza na nani.

Twiga Stars imemaliza mechi za Kundi B, ikiwa kinara kwa kushinda michezo yote mitatu. Iliichapa Zimbabwe mabao 3-0, ikashinda tena 2-0 dhidi ya Botswana kabla ya ushindi mwingine wa 3-0, dhidi ya Sudan Kusini, mabao yote kwenye mechi ya juzi yakifungwa na Stumai Athumani.

Ratiba ya michuano hiyo inaonyesha mshindi wa Kundi B atacheza na mshindi wa pili wa Kundi C, huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa Twiga Stars kucheza kati ya Zambia na Uganda, ambazo zinaongozana msimamo wa kundi hilo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**STERLING ATAKIWA BARCA**

BARCELONA wanafikiria uhamisho wa mshambuliaji wa Manchester City na England Raheem Sterling, 26. ***(Mundo Deportivo)***

**KASSIE MBADALA WA POGBA**

KLABU ya Manchester United inafikiria kumpata kiungo wa kati wa AC Milan, Franck Kessie, 24, kama mbadala wa Paul Pogba. ***(Calcio Mercato)***

**INTER YAPANGA KWA ALONSO**

INTER Milan wako tayari kurejesha nia yao ya kumpata beki wa pembeni wa Chelsea, Marcos Alonso, 30, raia wa Hispania. ***(Tutto Mercato)***

**TORRES KUTUA MAN CITY**

KLABU ya Manchester City wapo katika mbio za kumnasa mlinzi wa Villarreal na Hispania, Pau Torres, 24. ***(Metro)***

**XAVI KUMRITHI KOEMAN**

BARCELONA wamebaki kwenye mazungumzo na kiungo wa kati wa zamani wa Hispania, Xavi mwenye, 41, kuhusu kuchukua nafasi ya kocha Ronald Koeman. ***(90min)***

**YAMFUNGUKIA DE BEEK**

EVERTON ilijaribu kumsajili Donny van de Beek, 24, kwa mkopo kutoka Manchester United na ingependa kumchukuwa kiungo huyo wa kati wa Uholanzi katika dirisha la usajili la Januari. ***(NOS via Mail)***

**NUNO KUFUKUZWA SPURS**

TOTTENHAM Hotspur inaweza kumtimuwa kocha Nuno Espirito Santo, bila kulipa fidia yoyote ikiwa hatawaongoza kufikia nafasi sita za juu kwenye Ligi Kuu England. ***(Athletic)***

**KOZLOWSKI HATAKI MASTAA**

KIUNGO wa kati wa Pogon Szczecin, Kacper Kozlowski, 17, ambaye amekuwa akifuatiliwa na Liverpool, AC Milan na RB Leipzig, amesema havutiwi na "majina makubwa". ***(Sport Interia)***

**SOUTTAR ATAKIWA EVERTON**

KOCHA wa Everton, Duncan Ferguson, alikwenda kumfuatilia mlinzi wa kati wa Stoke City, Harry Souttar, 22, wakati 'Toffees' hao wakipanga uwezekano wa kuondoka kwa Yerry Mina. ***(Sun)***

**DAU LA TCHOUMENI LAANIKWA**

MONACO imetangaza dau la pauni milioni 34 kwa kiungo wa kati, Aurelien Tchouameni, 21, anayewaniwa na Juventus na Chelsea. ***(Calciomercato)***

**GONZALEZ MTEGONI CITY**

KLABU ya Manchester City wanamfuatilia kiungo wa kati wa Hispania, Nico Gonzalez anayekipiga Barcelona, ambaye hajapewa nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza. ***(Fichajes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ATOA SIRI YA CHOZI LA REAL MADRID

**●●● Kuondoka ndilo lililokuwa chaguo langu, tamaa yangu ilikuwa wazi majira ya joto, nililia pale...**

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint Germain, Kylian Mbappe, amekubali kuwa alitaka kujiunga na Real Madrid kipindi cha dirisha la usajili la majira ya joto kabla ya dili hilo kushindikana mwishoni.

Mchezji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, alihusishwa na kujiunga na miamba ya hiyo ya Madrid baada ya kukataa kuongeza mkataba wake na matajiri wa jijini Paris.

Real Madrid walipeleka ofa mbili ambazo kwa mchezaji huyo mwenye miaka 22, zilikataliwa katika siku za mwishoni kwenye dirisha la majira ya joto ingawa Mbappe aligomea mkataba mpya.

**PSG bado wana nia ya kumbakisha mchezaji huyo wa zamani wa AS Monaco, huku nyota huyo akithibitisha kuwa alikuwa anahitaji kujiunga na miamba hiyo ya Madrid msimu wa 2021/22.**

"Kuondoka ndilo lililokuwa chaguo langu, tamaa yangu ilikuwa wazi majira ya joto, nimejifunga na PSG, na kama ningeondoka majira ya joto, basi ningeenda Real Madrid tu, nililia pale nilipojua kuwa siwezi kwenda Madrid," alisema Mbappe akinukuliwa na jarida la France Football.

Mbappe tayari amefunga mabao manne katika mechi tisa kwenye Ligue 1 hadi sasa ni sehemu ya nyota wanaotegemewa na kocha Mauricio Pochettino pembeni ya Neymar na Lionel Messi ambaye alijiunga na klabu hiyo mapema majira ya joto msimu huu.

MECHI KALI
HOME
ITALY
2.34 | 3.10 | 3.34
SPAIN
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 559

# ABRAHAM, CHILWELL WAONGEZWA ENGLAND



**LONDON,** England

KOCHA Gareth Southgate amewajumuisha Tammy Abraham na Ben Chilwell kwenye kikosi chake cha England kuelekea michezo iliyopo mbele yao ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Andorra na Hungary, wakati Reece James akijiondoa kutokana na kuwa majeruhi.

Chilwell beki wa kulia atajiunga na kikosi hicho cha 'Simba Watatu' akichukua nafasi ya James, huku Abraham akienda kuongeza nguvu kwenye nafasi ya ushambuliaji.

Abraham ambaye aliondoka Chelsea majira ya joto kujiunga na AS Roma hadi sasa amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho tatu katika michezo 10 kwenye klabu yake mpya.

Chilwell alikuwa kikosi cha England kwenye Euro 2020, lakini hakuichezea hata dakika moja timu hiyo wakati ikifika fainali, wakati mara ya mwisho Abraham kuitwa kwenye kikosi cha Simba Watatu hao ilikuwa ni Novemba mwaka jana.

England watacheza na Andorra ugenini Oktoba Jumamosi wiki hii kabla ya kukipiga na Hungary kwenye uwanja wa nyumbani, Wembley Jumanne ijayo.



# *Ranieri apewa miaka 3 Watford*

**LONDON,** England

CLAUDIO Ranieri amesaini mkataba wa miaka mitatu kuinoa Watford akichukuwa mikoba iliyoachwa na Xisco Munoz kwenye viunga vya pale Vicarage Road.

Ranieri mwenye umri wa miaka 69, anakuwa kocha wa 13 tangu familia ya Pozzo ichukue umiliki wa klabu hiyo mwaka 2012.

Kocha huyo aliiongoza Leicester City kwenye safari ya mafanikio na kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2016, hivyo kubaki kuwa na msimu mrefu zaidi wa mafanikio.

Sasa amerudi kwenye mikikimikiki ya Ligi Kuu England baada ya kuwa nje ya Uingereza kwa miaka miwili.

Ranieri pia alikuwa na msimu mbaya akiwa na Fulham mwaka 2019, ambapo alishinda michezo mitatu tu kati ya 17 kwenye viunga vya Craven Cottage kabla ya kupokewa na msaidizi wake, Scott Parker.

Bodi ya Watford inaamini kuwa Ranieri ni mtu sahihi kuiongoza timu hiyo msimu huu, baada ya klabu hiyo kushinda michezo miwili kati ya saba katika kuwania nafasi za juu.

# 9,183,880 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/10/21 | 17:00 | Lugo vs Girona | 2.95 | 2.95 | 2.51 |
| 02. 09/10/21 | 17:00 | Hartlepool vs Northampton | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 03. 09/10/21 | 17:00 | Bristol Rovers vs Carlisle | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 04. 09/10/21 | 17:00 | Stevenage vs Exeter | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 05. 09/10/21 | 17:00 | Sutton United vs Port Vale | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 06. 09/10/21 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 09/10/21 | 17:00 | Newport vs Bradford City | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 08. 09/10/21 | 17:00 | Boreham Wood vs Dagenham and Redbridge | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 09. 09/10/21 | 22:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.70 | 2.94 | 2.75 |
| 10. 10/10/21 | 08:00 | Matsumoto Yamaga vs Tochigi SC | 2.61 | 2.86 | 2.76 |
| 11. 10/10/21 | 15:00 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 12. 10/10/21 | 19:15 | Alcorcon vs Burgos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 13. 10/10/21 | 22:00 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.63 | 2.88 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 06 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2777 | Urawa Red Diamonds vs Cerezo Osaka | 1.99 | 3.20 | 3.59 |
| 13:00 | 5251 | Nagoya Grampus vs FC Tokyo | 1.96 | 3.06 | 3.88 |
| 13:00 | 5574 | Vanraure Hachnohe FC vs Kataller Toyama | 3.82 | 3.39 | 1.86 |
| 13:00 | 5718 | Incheon Utd vs Gangwon | 2.86 | 3.05 | 2.39 |
| 14:00 | 4082 | Bangkok Utd vs Prachuap FC | 1.37 | 4.64 | 6.58 |
| 14:00 | 4621 | Bangkok Glass vs Chiangrai Utd | 1.70 | 3.67 | 4.25 |
| 14:45 | 5250 | Balestier Khalsa vs Hougang United | 4.46 | 4.27 | 1.57 |
| 15:00 | 1396 | Buriram Utd vs Pattaya United FC | 1.40 | 4.54 | 6.19 |
| 15:00 | 2033 | Khon Kaen United FC vs Nakhon Ratchasima | 2.85 | 3.19 | 2.32 |
| 16:00 | 3054 | FK Buducnost Dobanovci vs FK Loznica | 2.85 | 3.00 | 2.65 |
| 16:00 | 3751 | FK Zlatibor vs FK Zarkovo | 2.04 | 2.91 | 3.83 |
| 16:30 | 2948 | Varnsdorf vs Zbrojovka Brno | 2.87 | 3.35 | 2.23 |
| 16:30 | 3393 | Dukla Prague vs Ceske Budejovice | 3.49 | 3.44 | 1.93 |
| 17:30 | 3321 | Nosaby IF vs IFK Karlshamn | 2.27 | 3.43 | 2.75 |
| 18:00 | 2192 | Jordan vs Malaysia | 1.40 | 4.69 | 7.59 |
| 18:00 | 2558 | Linense vs Cordoba | 1.62 | 3.74 | 4.76 |
| 18:00 | 3842 | Al Khaleej Club vs AL Khlood | 1.67 | 3.63 | 4.55 |
| 18:00 | 5910 | CD Ebro vs Hercules CF | 1.91 | 3.39 | 3.63 |
| 18:10 | 2782 | Alshoulla vs Ohud Medina | 1.89 | 3.53 | 3.53 |
| 19:00 | 1101 | Sudan vs Guinea | 4.25 | 3.24 | 1.82 |
| 19:00 | 2768 | UP Langreo vs Real Aviles | 1.91 | 3.50 | 3.50 |
| 19:00 | 2794 | Backa Palanka vs Macva Sabac | 2.57 | 2.91 | 2.76 |
| 19:00 | 4551 | Leioa vs Alondras CF | 1.81 | 3.49 | 3.88 |
| 19:00 | 4665 | Bahrain vs Curacao | 1.72 | 4.00 | 4.39 |
| 19:00 | 5076 | Racing Santander vs Arenas De Getxo | 1.44 | 4.36 | 5.81 |
| 19:00 | 5359 | RS Gimnastica de Torrelavega vs Alfaro CD | 2.01 | 3.33 | 3.38 |
| 19:00 | 5402 | Guijuelo vs Toledo | 3.15 | 3.25 | 2.13 |
| 20:00 | 2389 | Varbergs Gif FK vs Vinbergs IF | 1.74 | 4.35 | 3.43 |
| 20:00 | 3188 | Tromsdalen vs Floya | 1.11 | 8.13 | 13.55 |
| 20:00 | 3848 | Mallorca B vs CD Llosetense | 1.48 | 4.04 | 5.78 |
| 20:00 | 4435 | CSD Comunicaciones vs Club Xelaju | 1.52 | 3.83 | 5.63 |
| 20:00 | 4654 | CD Artistico Navalcarnero vs CF Villanovense | 2.54 | 3.27 | 2.54 |
| 20:05 | 1943 | Jeddah Club vs AL Kawkab | 2.15 | 3.55 | 3.20 |
| 20:30 | 5414 | Skellefteaa FF vs Bodens BK | 2.57 | 3.78 | 2.27 |
| 20:45 | 3512 | FC Arlanda vs Sandvikens AIK FK | 4.64 | 4.73 | 1.50 |
| 20:45 | 3705 | FA 2000 vs Kolding IF | 4.45 | 3.38 | 1.74 |
| 21:00 | 1464 | Llagostera vs Izarra | 1.62 | 3.74 | 4.76 |
| 21:00 | 2557 | IFK Osteraakers FK vs Kvarnsvedens IK | 1.77 | 3.83 | 3.74 |
| 21:00 | 3274 | Lleida Esportiu vs SD Ejea | 2.01 | 3.33 | 3.38 |
| 21:00 | 4782 | UD Collerense vs CF Soller | 2.54 | 3.27 | 2.54 |
| 21:15 | 3115 | Yeclano Deportivo vs Melilla | 3.38 | 3.33 | 2.01 |
| 21:30 | 3630 | Real Murcia vs Xerez CD | 1.35 | 5.02 | 6.38 |
| 21:45 | 2111 | Italy vs Spain | 2.34 | 3.10 | 3.34 |
| 22:00 | 2104 | Brasil Pelotas RS vs Operario PR | 3.67 | 2.70 | 2.21 |
| 22:00 | 3480 | Morocco vs Guinea Bissau | 1.21 | 5.43 | 11.64 |
| 22:00 | 3763 | Tigres FC (COL) vs Real Cartagena | 2.38 | 2.83 | 3.12 |
| 23:00 | 5757 | LDU Portoviejo vs Chacaritas FC | 2.03 | 3.30 | 3.35 |
| 23:30 | 1524 | CD Duros Del Balon vs Cumbaya FC | 2.09 | 3.25 | 3.25 |
| 23:30 | 2155 | America vs CD Alianza Cotopaxi | 2.09 | 2.96 | 3.59 |
| 23:30 | 2323 | Puerto Quito vs Guayaquil SC | 2.21 | 3.05 | 3.55 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# OLKJAER ADO 'YUPO UPO' SANA NITED



**ANCHESTER,** England

MABOSI wa Klabu ya Manchester United hawana mpango wa kumfukuza Kocha Mkuu, Ole Gunnar Solkjaer licha ya kuwa na wenendo mbovu hivi karibuni, kwa mu- u wa Daily Mail.

Tayari ndani ya msimu wa 2021/22, ameteza mechi tatu na amelazimisha sare bili huku akipata ushindi katika mechi no katika michuano yote.

Jina lake limekuwa likitajwa kuwa moja ya akocha watakaofukuzwa mapema kutoka- na mabosi na timu hiyo kuwekeza nguvu bwa kwenye usajili wa nyota wakubwa iki- ni pamoja na Cristiano Ronaldo ili aweze wapa matokeo ila mambo yamekuwa ni agumu.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa licha ya matokeo wa mabaya na mwendo mbovu wa timu vo iliyo nafasi ya nne kwenye msimamo wa gi Kuu England pamoja na pointi zake 14 ku vinara wakiwa ni Chelsea wenye pointi bado mabosi hawana mpango wa kum- a kazi kwa kuwa wanaona anafanya vizuri.

Anayetajwa kupewa mikoba ya Solkajaer Antonio Conte ambaye kwa sasa yupo ru kwa kuwa hawafundishi tena Inter Mi- n ambao aliwapa ubingwa walioukosa kwa uda mrefu.



# Coutinho sasa kutua EPL

**LONDON,** England

KIUNGO wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho, atatua Ligi Kuu England (EPL), kwa sababu Arsenal na Tottenham Hotspur zipo kwenye mazungumzo ya kuipata saini yake.

Barca ipo tayari kumuuza Coutinho kwa sababu hali yao kiuchumi si nzuri na mshahara wa nyota huyo wa pauni 200,000 kwa wiki unazidi kuiweka bajeti yao njiapanda.

Tangu kuanza kwa msimu huu, Coutinho amecheza dakika 82 pekee za michuano yote ikiwa ni baada ya kurejea kutoka kwenye majeraha yaliyokuwa yanamsumbua tangu msimu uliopita.

Coutinho amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza tangu atue kwenye viunga hivyo vya Camp Nou mwaka 2018 kwa dau la pauni milioni 145 lililovunja rekodi ya mauzo kwa upande wa Ligi Kuu England.

Taarifa zinadai mchezaji huyo angependa zaidi kurejea Liverpool, lakini wababe hao hawajaonyesha mpango wa kumchukua kiungo huyo wa ushambuliaji aliyewahi kushinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu mfululizo kuanzia mwaka 2014 hadi 2016.

Kiungo huyo aliwahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa mwaka 2020 akiwa na Bayern Munich aliyokuwa anaitumikia kwa mkopo na kwenye mchezo wa nusu fainali dhidi ya Barca alifunga mabao mawili.

Michezo
Jumatano Oktoba 6, 2021
Nipashe



Mbappe atoa siri ya chozi la Real Madrid UKURASA 21

CHAMBUA...



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Kibu Denis akipiga hesabu ya kuwachambua mabeki wa timu hiyo wakati wa mazoezi yaliyofanyika juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kujiandaa na mechi ya dhidi ya Benin kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022, itakayopigwa kesho uwanjani hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samatta, Msuva wainogesha Stars

## ●●● Mtihani sasa kwa Poulsen kuamua kuanza na wote pamoja Kibu, Bocco, Benin watua usiku...

**Na Mwandishi Wetu**

WASHAMBULIAJI tegemeo wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta na Simon Msuva wanaocheza soka la kulipwa nchini Ubelgiji na Morocco, wameinogesha kambi ya timu hiyo ya taifa baada ya kujiunga na wenzao kambini kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022 dhidi ya Benin.

**Samatta na Msuva walitua juzi usiku na kujiunga moja kwa moja na wenzao kambi tayari kwa mchezo huo utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kabla ya kurudiana nchini Benin Jumapili wiki hii.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, alisema tayari wachezaji wote wamewasili kambini akiwamo Samatta na Msuva kutoka Ubelgiji na Morocco.

"Wachezaji wote wamewasili kambini, kwa Samatta na Msuva waliwasili jana usiku [juzi], lakini Benin watawasili leo usiku [jana usiku] tayari kwa mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa," alisema Ndimbo.

Aidha, Ndimbo alisema kwa upande wa uongozi kila kitu kinaenda vizuri ikiwamo alichohitaji kocha Kim Poulsen na sasa kazi kubwa imebaki kwake kuhakikisha anatekeleza majukumu yake ili kufikia malengo yanayotarajiwa na Watanzania.

Tayari Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Poulsen amekiongezea kikosi chake nguvu kwenye safu ya ushambuliaji na ulinzi baada ya kumwongeza mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis kutokana na tatizo lake la uraia kutatuliwa huku pia akimjumuisha beki wa Yanga, Kibwana Shomari kuchukua nafasi ya Shomari Kapombe ambaye ni majeruhi.

Akizungumzia mchezo huo, Poulsen alisema anaamini mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wapinzani wao hao na muda mchache wa kujiandaa.

Poulsen alisema Benin inaundwa na wachezaji wengi wenye uzoefu wa mechi za kimataifa kutokana na kucheza soka Ulaya hususan Ufaransa tofauti na Taifa Stars ambayo kikosi chake kinajumuisha nyota wengi wanaocheza soka nchini.

Lakini kujiunga kwa Kibu Stars, sasa kunampa Poulsen wigo mpana katika uchaguzi wa safu yake ya ushambuliaji ambayo tayari ilikuwa na John Bocco na Samatta huku pia akiwa pia na chaguo pana katika safu ya viungo washambuliaji ambayo ina Feisal Salum 'Fei Toto', Novatus Dismas, Msuva, Iddy Suleiman 'Nado,' Riliant Lusajo na Abdul Hamisi Suleiman.

Taifa Stars inaongoza Kundi J katika mechi hizo za kufuzu ikiwa na pointi nne sawa na Benin ikifuatiwa na DR Congo yenye alama mbili huku Madagascar ikiburuza mkia bila pointi.

## Gomes na hesabu kali za Simba CAF

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi cha Simba, tayari kimeingia kambini huku wachezaji wakipewa dozi ya mazoezi kutwa mara mbili, asubuhi na jioni, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes, amesema hana wasiwasi kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy FC ya Botswana.

Simba imeingia kambini juzi ikiwa na wachezaji pungufu baada ya nyota wake 16 kuitwa timu zao za taifa kuelekea mechi za kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema hawataidharau Jwaneng Galaxy katika mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika na badala yake wanajiandaa kikamilifu kukabiliana nao.

Alisema ana kikosi imara na wachezaji wazuri ambao wanauwezo wa kupambana kutafuta matokeo hali ambayo anajivunia, hivyo maandalizi mazuri yatawapa nafasi ya kufanya vizuri.

"Mbali ya mazoezi na masuala ya kiufundi tunayafanya mazoezini ili kushinda, nitakuwa na awamu moja ya kuongea na wachezaji wangu kabla ya mechi ili kujindaa kiakili kile ambacho wanakwenda kukutana nacho kutoka kwa wapinzani.

"Tumeingia katika mashindano makubwa, malengo yetu ni kuona tunasonga mbele tulipoishia msimu uliopita, kwa hakika tunahitaji kucheza nusu fainali ya michuano hii," alisema Gomes.

Aidha, Gomez alisema licha ya kutoanza vizuri sana msimu mpya wa Ligi Kuu, lakini kwake anaona ni kawaida kutokea hasa kutokana na wachezaji wake wengi kutumika muda mrefu kwenye klabu na timu za taifa.

"Ni jambo la kawaida muda mwingine kuanza kwa sare au kufungwa.., kikubwa ni kurejea kwenye mstari na kufanya kile ambacho tumekuwa tukikifanyia mazoezi na kujiandaa nacho muda mrefu," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >